# Nipashe

Jumamosi Novemba 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581141

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS.1,053,232,366

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Mwinyi** ataka wataalamu wa maradhi ya figo

UKURASA 12




UKURASA 13

# Suluhu mgawo wa umeme yapatikana

UKURASA 4 & 9

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### SERIKALI KUGHARAMIA MAZISHI YA WANAFUNZI

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema amesema serikali inagharamia mazishi ya miili ya wanafunzi watatu waliofariki dunia katika ajali ya moto iliyotokea kwenye Kituo Jumuishi ...

## Waziri: Hakuna wilaya itakayokosa chakula cha msaada

UKURASA 9



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, akiwa na Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, wakikagua bweni la watoto wenye ulemavu lililoteketea kwa moto katika kituo cha Buhangija na kusababisha vifo vya watoto watatu, walipotembelea shuleni hapo juzi jioni. **PICHA: MARCO MADUHU**



Angela Kizigha



Adam Malima



Angelina Mabula



Dk. Edmund Mndolwa

## Vigogo zaidi wabwagwa uchaguzi CCM

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA SC, MBEYA CITY MECHI YA KIWANGO LEO UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akiongozana na Spika wa Bunge mstaafu Mzee Pius Msekwa (kushoto) na mkewe Anna Abdallah (katikati), baada ya kuwasili nyumbani kwake Wilaya ya Ukerewe, mkoani Mwanza, kwa ajili ya kumjulia hali, akiwa katika ziara wilayani humo jana. **PICHA: OMR**

# Vigogo wazidi kubwagwa uchaguzi wa ndani CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BAADHI ya vigogo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliogombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya Jumuiya ya Wazazi, wamebwagwa akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti Dk. Edmund Mndolwa.

Vigogo wengine walioshindwa ni Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dk. Angelina Mabula, na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, waliogombea nafasi ya wajumbe watatu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC).

Akitangaza matokeo hayo jana jijini Dodoma, Msimamizi wa Uchaguzi huo, Maalim Kombo Hassan, alimtangaza Fadhil Maganya aliyeshinda kwa kura 578 akimwacha mbali Dk. Mndolwa aliyepata kura 64.

Katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti, Doto Iddi Mabrouk alitangazwa kuwa mshindi kwa kupata kura 530 kati ya 736 zilizopigwa akiwashinda wagombea wengine wanne.

Hassan aliwatangaza washindi wa nafasi ya wajumbe wa NEC, Tanzania Bara, Hamoud Abuu Jumaa aliyepata kura 569, Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko aliyepata kura 535 na George Gandye kura 238.

Katika nafasi hiyo, walioshindwa ni Dk. Mabula alipata kura 232 huku Malima akipata kura 195.

Kwa upande wa Baraza Kuu kundi la Zanzibar, msimamizi huyo aliwatangaza Christina Antony, aliyepata kura 325, Ally Issa Ally kura 397 na Time Bakari kura 441 kuwa ndio washindi wa nafasi hizo.

Wajumbe waliochaguliwa Baraza Kuu Tanzania Bara ni Ally Kassim Mandai, aliyepata kura 220, Lulu Abas Mtemvu kura 248 na Saad Mohammed Khimji kura 298.

Naye Peter Kasera aliibuka mshindi wa uwakilishi Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) kwa kupata kura 264 na kwa upande wa uwakilishi wa UWT aliyeibuka mshindi ni Asha Juma Ferouz aliyepata kura 287 akiwashinda wagombea wengine watatu.

Dk. Mndolwa akizungumza mara ya kushindwa kutetea nafasi yake, aliwashukuru wajumbe 64 waliompigia kura.

"Nimepata kura 64 siyo haba. Hilo sio tatizo kikubwa tumepata viongozi wapya 'tuwasupport' (tuwaunge mkono). Nawashukuru wale wote niliofanya nao kazi katika kipindi cha miaka mitano," alisema.

Mwenyekiti mpya, Maganya, alisema hakutegemea kupata ushindi huo, na hiyo ni sawa na ameokota embe aina ya dodo chini ya mti wa mpilipili.

"Ndugu wajumbe mimi nimewiwa, nimehemewa, kwa namna ambavyo nimepigiwa kura mmenipa heshima. Kwa kweli mmefanya maajabu na wajumbe wa wazazi mmevunja rekodi," alisema.

"Wanasema wajumbe hawafai lakini leo mmefaa mmetengeneza historia. Ndugu zangu nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisiposema nimeokota dodo katika mti wa mpilipili sikutegemea, mimi sina jina lakini nimeshinda." Aliongeza.

Mwenyekiti huyo aliweka wazi tamanio lake kwa jumuiya hiyo ni kuwa na hospitali kubwa ya rufani ambayo itatoa tiba kwa Watanzania.

"Nataka tuwe na Wazazi Commercial Bank, wakfu kwa wazazi kazi yake itakuwa kushawishi misaada, uwezo ninao maarifa ninayo tunaenda kutekeleza haya," alisema mwenyekiti huyo.

Alitaja kipaumbele chake kingine ni ufugaji wa kisasa ambao utaibadilisha kiuchumi jumuiya hiyo.

"Ninajua watumishi zipo kero mbalimbali sioni sababu nitashirikiana na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, kuziweka wazi, zinatatulika tu," alisisitiza.

# Utouh asema bila uwazi, uwajibikaji hakuna tija

**Augusta Njoji na Marco Maduhu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, amesema bila uwazi na uwajibikaji kwenye sekta ya madini, nishati, mafuta na gesi asilia hakutakuwa na tija kwa Watanzania.

Utouh ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika sekta ya uziduaji (MSG), aliyasema hayo jana katika Jukwaa la Uziduaji lililoshirikisha wadau wa madini wakiwamo wachimbaji lililoandaliwa na Taasisi ya HakiRasilimali jijini hapa.

Alisema kamati hiyo inatekeleza sheria ya TEITI ambayo inataka kampuni zinazojihusisha na masuala ya uziduaji kuwa na uwazi na kuwajibika.

Akizungumza katika mada ya uwazi na uwajibikaji, alisema uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini, nishati, mafuta na gesi asilia, kwenye nchi nyingi zenye rasilimali hiyo bila kuwepo na utaratibu mzuri wa usimamizi huwa hazina tija kwenye nchi.

"Kila mwaka TEITI tunataka tupewe taarifa ya malipo yote ambayo wameyafanya kwenye serikali na taasisi zake zote, na tunaitaka serikali itupe taarifa ya malipo yote tuliyopokea kutoka kwenye kampuni hizo halafu tunafanya ulinganisho, tumeona kila mwaka sasa hivi mambo yanaongezeka ambapo kwa miaka minne au mitano iliyopita uchangiaji wa sekta hii kwa uchumi wa nchi ilikuwa asilimia 3.2," alisema.

Alisema ifikapo mwaka 2025 matarajio na mipango ya serikali sekta hiyo ichangie kwa asilimia 10 na kwamba hawatafika huko kusipokuwepo na uwazi na uwajibikaji wa kweli katika usimamizi wa sekta hiyo.

"Jukwaa hili limezungumzia sana umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo ya taifa, rasilimali zilizopo ni za watanzania ni vizuri kuhakikisha zinasimamiwa kwa manufaa ya watanzania wote,"alisema.

Alisema tangu kuanza kutoa ripoti za TEITI mpaka sasa ripoti 12 zimetolewa zinazoonyesha kuwapo mafanikio makubwa katika sekta ya madini ikiwamo ongezeko la mapato na kuweka uwazi mchango wa kampuni za madini kuhusu wajibu wao kwa jamii (CSR).

"Mpaka sasa tumeshatoa ripoti 12 na zimeonyesha kuwapo mafanikio ingawa bado kuna changamoto ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi na kabla ya juni mwaka 2023 tutatoa taarifa ya 13," alisema.




Wadau wanaopambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, wakiandamana kuelekea kwenye viwanja vya Klabu ya Leaders Kinondoni, Dar es Salaam jana, kushiriki uzinduzi wa kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, ambazo kilele chake kitakuwa Desemba 10 mwaka huu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Msako vitendo vya ukatili waelekezwa vibanda umiza

**Na Romana Mallya**

SERIKALI kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WILDAF) imezindua kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia, ikibainisha kuwa msafara maalum utatumia siku 16 kupita mikoa mbalimbali kuhamasisha jamii kutokomeza vitendo hivyo.

Msafara huo utatembelea jamiii, shuleni, vituo vya mabasi na maeneo ambayo yanaonyesha kombe la dunia vikiwamo 'vibanda umiza' ili kuwafikia wanaume wengi zaidi na kuhamasisha mabadiliko ya kifikra, kimtazamo na matumizi mabaya ya mamlaka walizonazo katika kulinda wanawake na watoto.

Msafara huo pia utatembelea shuleni kujadiliana na watoto, walezi na walimu kuhusu mbinu mbalimbali za kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizungumza jana mkoani Dar es Salaam katika uzinduzi wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ulioandaliwa na WILDAF kwa kushirikiana na wizara, alisema ni lazima vitendo hivyo vitokomezwe.

Msafara huo maalum uliozinduliwa utatumia siku hizo 16 kuanzia jana hadi Desemba 10 mwaka huu kupita mikoani kutoa elimu.

Waziri Gwajima alisema: "Nimefahamishwa kwamba kwa uzito wa kampeni za mwaka huu, mmeandaa programu mbalimbali zikiwamo Msafara wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia ambapo nitauzindua leo (jana).

"Lengo la msafara huu ni kufikia jamii, mtu binafsi, wanafunzi na kuhamasisha mbinu mbalimbali za kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia. Nitashiriki kwenye baadhi ya mikoa ambayo msafara utapita."

Mkurugenzi Mtendaji wa WiLDAF, Wakili Anna Kulaya alisema kinachosikitisha ni kwamba wanaofanya vitendo vya ukatili, jamii inawafahamu na mara nyingi imekuwa ikiwalinda na kuamua kumaliza kesi nyumbani au kutotoa taarifa mapema na kutoa mwanya kwa watuhumiwa kurudia makosa.

Alisema hali hiyo inaleta madhara makubwa zaidi na hata kifo na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi na juhudi za serikali za kufikia usawa wa kijinsia na maendeleo endelevu.

Alisema hiyo ndiyo sababu Mtandao wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI) umedhamiria mwaka huu kwa kushirikiana na wizara kufanya kampeni hiyo kubwa itakayoshirikisha mtu mmoja mmoja, familia, wazazi na walezi, jamii na taasisi kwa ujumla.

"Tunatumia kampeni hii kupaza na kukemea vitendo vya ukatili na mauaji dhidi ya wanawake kwani vinazuilika. Jamii bila ukatili na mauaji dhidi ya wanawake inawezekana. Tuvunje ukimya na tuchukue hatua. Kwa pamoja tunaweza kuokoa maisha ya wanawake na watoto," alisema.

Aliongeza kuwa MKUKI na wadau wengine wamejipanga kutumia siku 16 za kampeni kufanya shughuli mbalimbali kuongeza ushiriki wa kila mwanajamii katika kutokomeza ukatili wa kijinsia.

"Kwa leo (jana) utazindua msafara wa kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia ambao utapita mikoa mbalimbali ikiwamo Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Shinyanga, Geita, Mara na Arusha ukihamasisha jamii kuungana nasi katika kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia." alisema.

Pia alisema kwa kuwatumia bodaboda, watahamasisha wawe mabalozi wa kupinga vitendo vya ukatili pamoja na kuokoa wanawake na watoto dhidi ya ukatili.

"Desemba 8 (mwaka huu) tunategemea kuwa na tuzo maalum kwa vinara wanaolinda wanawake, watoto na kuzuia ukatili wa jinsia," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Amos Mpanju alisema pasipo kuhusisha wanaume, ukatili utaendelea kuwa janga, akitoa angalizo kuwa kuna haja kutenganishwa tendo la ndoa na ndoa kama taasisi ili kupinga vitendo vya ukatili vinavyosababishwa na uhusiano.

"Viongozi wa dini wawe na uamuzi wa kuwaelekeza vijana kabla ya kuingia katika ndoa, wasimamizi wa ndoa wana wajibu maalum kuhakikisha ndoa wanazosimamia zinasimama, lakini sasa wasimamizi wa ndoa wanaangaliwa kwa maumbo na mwonekano wao, ndoa nayo isiwe fasheni kuangalia maumbo," alionya.

# 'Mgawo wa maji Dar, Pwani sasa umekwisha'

**Na Frank Monyo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ametangaza kumalizika kwa mgawo wa maji katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani baada ya mvua kuanza kunyesha na kusababisha maji kuongezeka katika Mtambo wa Ruvu Chini na Ruvu Juu.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ilikuwa inazalisha lita milioni 520 kipindi cha ukame lakini sasa inazalisha lita milioni 590 na mahitaji ya maji kwa wakazi Dar es Salaam ni lita milioni 544, hivyo kuwa na ziada ya lita milioni 46.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kwenye Mtambo wa Ruvu Chini wakati wa ukaguzi wa mtambo huo, Makalla alisema mikoa hiyo ilikumbwa na mgawo wa maji uliosababishwa na ukame uliotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kutokana na shida hiyo, jitihada mbalimbali zilifanyika ikiwamo kuondoa watu wanaofanya shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji na kufufua visima vya dharula 162 mkoani Dar es Salaam vilivyosaidia kupunguza makali ya mgawo wa maji.

"Leo (jana) tumefika hapa (Ruvu Chini) kukagua chanzo cha maji, maji yamerejea katika hali ya kawaida na zaidi, kwa hiyo nitamke rasmi kuwa mgawo wa maji Dar es Salaam sasa hakuna.

Alisema Mtambo wa Ruvu Juu unazalisha lita milioni 196 na Ruvu Chini lita milioni 270 na kufanya kuwe na lita milioni 466.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja aliwashukuru viongozi wa dini kwa maombi waliyoyafanya hivi karibu ili mvua inyeshe.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**26 - 11- 2022**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe 01-12-2022 hadi 08-12-2022 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA gari hizo zina namba za usajili:

| | | |
|---|---|---|
| **T 458 DYG /T 380 DHQ** | **T 973 DTN /T 377 DHQ** | **T 967 DTN /T 153 CHN** |
| **T 681 DUB /T 881 EAU** | **T 454 DYG /T 877 EAU** | **T 460 DYG /T 879 EAU** |

2. Njia itakayotumika: BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia MOROGORO ROAD. Gari zitasafiri muda wa usiku **(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)** Kutoka Dar es Salaam Port mpaka Mlandizi

Kutoka Mlandizi kwenda Uyole gari zitasafiri muda wa mchana ( **kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)
Kutoka Uyole Mpaka Mbalizi Gari zitasafiri muda wa usiku **(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)**
Kutoka Mbalizi kwenda Tunduma gari zitasafiri muda wa mchana ( **kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

17167402

**Form 360a**
**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY**
**Notice of Appointment of Liquidator: Voluntary Winding-Up**
**Pursuant to section 360 of the Companies Act 2002**

To the Registrar of Companies

Company Number: **138686183**

Company Name (in Full): **TEMPLARS LIMITED**

I-: (name(s)): **JOSEPH NICAS LUKOA**

of: **P.O BOX 18040, DAR ES SALAAM**

(address(es)): **MIKOCHENI B, HOUSE NO. 58, KANISANI ROAD, KINONDONI, DAR ES SALAAM.**

give notice that on 22nd October 2022
I was appointed a liquidator of the above named company.
The appointment was by the company
Type of Liquidation: Members
Signed ______ Date 22nd October 2022
NAME IN BLOCK LETTERS: **JOSEPH NICAS LUKOA**

FOR OFFICIAL USE ONLY.

17166702

# Suluhisho mgawo umeme lapatikana

**Na Salome Kitomari**

WIZARA ya Nishati imetia saini mkataba wa uzalishaji na ugawanaji mapato (PSA) wa Kitalu cha Ruvuma kitakachozalisha gesi asilia futi za ujazo bilioni 466 kilichoko chini ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na kampuni ya Ndovu Resources.

Gesi hiyo inatarajiwa kuongeza umeme kwenye Gridi ya Taifa kwa asilimia 60 ili kuwa na nishati ya uhakika nyakati zote.

Akizungumza katika halfa ya kutia saini mkataba huo jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Nishati, January Makamba alisema kitalu hicho kina leseni mbili za Lindi na Mtwara na kwamba Oktoba mwaka huu kampuni hiyo iliuza asilimia 50 ya hisa zake kwa kampuni ya ARA Petroleum Ltd na ARA kuwa mwekezaji mkuu.

"Ndugu zangu wa Lindi na Mtwara sasa nchi yetu imeanza kuingia kwenye uchumi wa gesi, sio kwa tukio hili la leo, bali kwa mlolongo wa matukio na jitihada za serikali. Arusha tupo hatua ya mwisho ya majadiliano mradi wa kuchakata gesi wa zaidi ya Sh. trilioni 70, ni uwekezaji mkubwa barani Afrika," alisema.

Waziri huyo alisema mkataba huo ulikuwa na vifungu vinavyosimamia mapato iwapo mafuta yatagunduliwa katika kitalu husika, kwa kuwa mwekezaji amegundua gesi asilia mkataba wa nyongeza umeandaliwa, ili kuongeza vifungu vinavyosimamia mapato ya gesi asilia.

"Leo (jana) tunafanya hafla ya uwekaji saini katika mkataba wa nyongeza wa mkataba wa awali wa uzalishaji na ugawanaji mapato wa Kitalu cha Ruvuma baada ya kukamilika kwa majadiliano baina ya timu ya majadiliano ya serikali na wawekezaji," alifafanua.

Kwa mujibu wa January, hadi sasa visima viwili vimechorongwa katika kitalu hicho na kugundua gesi asilia kiasi cha futi za ujazo bilioni 466 na kwamba tafiti zinazoendelea zinanyesha kuna futi za ujazo bilioni 1,642.

"Kusainiwa kwa mkataba huu wa nyongeza ni hatua kubwa katika maandalizi ya kuendeleza gesi iliyogunduliwa na hivyo kuongeza uzalishaji wa gesi asilia nchini," alisema.

Waziri huyo alisema katika mradi huo uwekezaji unakadiriwa kuwa takribani dola za Marekani milioni 500 katika kuendeleza gesi iliyogunduliwa.

"Katika uendelezaji na uzalishaji wa Kitalu cha Ruvuma, TPDC inatarajiwa kushiriki kwa asilimia 15. Utekelezaji wa mradi huu unatarajia kuzalisha ajira kwa watanzania pamoja na kukuza uchumi wa nchi yetu kutokana na kodi na tozo mbalimbali zitakazopatikana kutokana mauzo ya gesi," alifafanua.

Waziri huyo ambaye pia ni Mbunge wa Bumbuli, alitaja faida nyingine zitakazopatikana ni pamoja na matumizi ya gesi katika kuzalisha umeme ambayo kwa sasa gesi asilia inachangia zaidi ya asilimia 60 kwenye Gridi ya Taifa. "Utekelezaji wa mradi huu utaongeza kiasi cha umeme unaozalishwa kutokana na gesi asilia, kuendesha viwanda, kutumia majumbani pamoja na kwenye magari," alisisiza.

Juzi Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilieleza umma kuwa kuna upungufu wa megawati 300 hadi 350 kwa siku kwenye vyanzo vya kuzalisha nishati hiyo, hali iliyoongeza makali ya mgawo wa umeme.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande alisema kiasi cha maji kwenye vyanzo vya Kihansi, Kidatu, Mtera, Nyumba ya Mungu na Hale kimepungua kwa kiwango kikubwa, hali inayoathiri uzalishaji wa nishati hiyo.




Waziri wa Nishati, January Makamba (wa tatu kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk. James Mataragio (wa pili kulia), wakitiliana sania mkataba wa nyongeza wa uzalishaji na ugawanaji mapato (PSA) kitalu cha gesi cha Ruvuma na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ARA Petroleum, Erhan Saygi (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ndovu Resources, Charles Santos (kulia), jijini Dar es Salaam jana. Waliosimama ni wanasheria wa pande zote mbili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIRA yabanwa wanaopata majanga kutolipwa stahiki

**Na Farida Ramadhani,** MWANZA

SERIKALI imeiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) kuzichukulia hatua za kisheria ikiwamo kuzifutia leseni za kufanyabiashara, kampuni zinazoshindwa kuwalipa fidia wateja waliopata majanga.

Maagizo hayo yalitolewa jana na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande alipotembelea na kukagua mabanda ya maonyesho katika maadhimisho ya pili ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yanayoendelea katika viwanja vya Rock City Mall jijini Mwanza.

Alisema waathirika wamekuwa wakipata usumbufu wakati wa kudai fidia kwa kuwa hawalipwi kwa wakati na hata ukifika muda wanapolipwa fedha inakuwa imeshashuka thamani.

"Malalamiko mengi yamekuja wizarani kuhusu kampuni hizi za bima, ninaiagiza TIRA izichukulie hatua zile ambazo hazifuati sheria na taratibu," aliagiza Chande.

Pia aliitaka Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima kutoa suluhu kwa wakati na kwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali ya nchi na kuhakikisha kuwa kampuni za bima zinawajibika ipasavyo kwa matendo yake ili wahusika kupata haki zao kwa wakati.

Naibu waziri huyo pia aliiagiza Benki Kuu (BoT) kukutana na benki na taasisi za fedha mbalimbali nchini kutafuta suluhu ya kupunguza riba za mikopo ili wananchi wengi wanufaike na kujikwamua kiuchumi.

Chande alifafanua kuwa serikali imeshusha riba ya mikopo inayokopwa na taasisi hizo hadi asilimia tatu, lakini kiwango cha riba cha kuanzia asilimia tisa kwenda juu kinachotozwa na taasisi za fedha kwa wakopaji ni kikubwa kwa wananchi wa kipato cha chini.

Akizungumzia masoko ya mitaji na dhamana, Chande aliiagiza Mamlaka ya Soko la Dhamana na Mitaji (CMSA) kuongeza wigo wa elimu kwa umma kuhusu dhamana hizo na namna mwananchi anavyoweza kunufaika kwa kuwa uelewa ni mdogo.

Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha nchini kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja, alisema maadhimisho hayo hayatoi elimu pekee bali ni fursa adhimu kwa ajili ya kuchukua maoni na ushauri wa wananchi kuhusu maeneo mbalimbali ya huduma za fedha yanayotakiwa kuboreshwa.

Alisema maoni yaliyotolewa yamechukuliwa na yatafanyiwa kazi katika masuala ya kisera, taratibu na kutekelezaji ili kuhakikisha sekta ya fedha inakua kwa asilimia 80 ya Watanzania kupatiwa elimu ya fedha ifikapo 2025.

## Waliovamiwa tope la mgodi wapewa chakula

**Na Neema Sawaka,** KISHAPU

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Shinyanga umetoa msaada wa tani 10 za mahindi kwa kaya 149 zilizoathiriwa na tope la bwawa la mgodi wa Kampuni ya Diamond Williamson Ltd wilayani Kishapu.

Mbunge wa Viti Maalum mkoani Shinyanga, Lucy Mayenga akikabidhi chakula hicho kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali imetoa msaada huo, akibainisha kuwa kaya 38 zilizopoteza chakula na makazi bado zinaishi kwenye kambi ya mgodi huo.

Mayenga alisema tukio lililotokea Novemba 7 mwaka huu limeigusa serikali na kuhakikisha inatimiza wajibu wake wa kikatiba - ustawi wa wananchi.

Kaimu Meneja wa NFRA Kanda ya Shinyanga, Revocatus Bisama alisema wametoa tani 10 za mahindi ambazo zitagawiwa kwa wanaoishi kambini, tani tano zikitolewa kwa kaya 38 zinazohifadhiwa kambini na tani tano kwa ajili ya kaya 11 zilizopanga.

Meneja uhusiano kutoka kampuni hiyo, Bernad Mihayo aliishukuru serikali kwa kutoa msaada na kuonyesha utayari wake wa kushirikiana na wawekezaji katika kuisaidia jamii.

Mihayo alisema mgodi umeridhia kaya hizo kutoka kwenye kambi na kwenda kupanga huku ikizilipia kodi ya nyumba kwa kipindi cha miezi sita wakati ukiwajengea nyumba za kudumu.

"Mgodi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kishapu umeandaa mashamba na kuyalima kwa ajili ya kuja kuwagawia waathirika chakula kipindi cha mavuno," alisema Mihayo.




Machinga wakiwa wameacha meza ndani ya mtaro wa maji ya mvua, Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, huku wengine wakiwa wameweka biashara zao kwenye njia ya waenda kwa miguu, kitendo kinachosababisha usumbufu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# RC ataka uwazi zabuni maji, ujenzi barabara

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba ameziagiza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala ya Majisafi na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) kuweka wazi utaratibu wa kutoa zabuni ili kuondoa rushwa katika mchakato mzima wa kupata makandarasi wenye sifa.

Serukamba alitoa agizo hilo jana wakati wa utiaji saini baina ya makandarasi na TARURA watakaojenga barabara mkoani hapa katika hafla iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Alisema TARURA, TANROAD na RUWASA ni vyema zikaanza utaratibu wa kufanya tathmini baada ya kumaliza taratibu za kutoa zabuni kwa makandarasi ili kupima mchakato ulivyokwenda na kuona kama kulikuwa na makosa yaliyotolewa awali.

Serukamba alisema taarifa za utoaji zabuni zikiwa wazi walioshindanishwa wanaweza kuona utaratibu ulivyokwenda mpaka kupatikana washindi, hivyo kusaidia kuondoa rushwa katika mchakato mzima wa kupata makandarasi wenye sifa na ubora.

"Tukimaliza manunuzi yote kwa mwaka TARURA, TANROAD na RUWASA muwe na 'checklist' inayoonesha zabuni zilizofanyika na mchakato ulivyokwenda moja kumpatia mkandarasi, rushwa haiondolewi kibabe bali inaondolewa kwa mfumo," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka makandarasi waliopata zabuni ya ujenzi wa barabara mkoani Singida kufanya kazi kwa weledi na kukamilisha kazi kwa wakati kama walivyokubaliana katika mikataba yao. Alisema makandarasi wahakikishe wanaondoa kero za usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa mkoani hapa kwa kujenga barabara zenye ubora wa hali ya juu na kuzikamilisha kwa wakati ili wananchi waweze kurahisishiwa maisha yao.

Serukamba aliitaka TARURA kusimamia kikamilifu makandarasi hao waliopewa zabuni kwa kuwa serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 21.2 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mijini na vijijini na kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Mhandisi Tembo David, alisema wakala katika mwaka wa fedha umepanga kutengeneza barabara zenye urefu wa kilometa 944 na kujenga madaraja na vivuko 72.

Tembo alisema kwamba TARURA Singida imejipanga kufanya matengenezo ya kawaida ya barabara kwa urefu wa kilometa 483 na matengenezo ya sehemu korofi zenye urefu wa km 224 na matengenezo ya muda maalum yenye urefu wa km 237.

Pia alisema TARURA itatekeleza majukumu ya utenegenezaji wa madaraja na vivuko 72 na ujenzi wa barabara za kiwango cha lami zenye urefu wa kilimita 5.1 na kilomita 550 ambazo zitajengwa kwa kiwango cha changarawe na kilomita 388.9 kiwango cha udongo.

Siamen Kimaro, Mkurugenzi wa Kampuni ya Tanlite Labour Based Contractors, akizungumza kwa niaba ya makandarasi wenzake waliopewa zabuni, alisema watahakikisha wanafanya kazi kwa weledi na kumaliza kwa wakati huku akiahidi ubora mkubwa katika kazi waliyopata.

# Serikali kugharamia mazishi ya wanafunzi

**Na Neema Sawaka,**
SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema amesema serikali inagharamia mazishi ya miili ya wanafunzi watatu waliofariki dunia katika ajali ya moto iliyotokea kwenye Kituo Jumuishi cha Walemavu Buhangija.

Wanafunzi waliofariki dunia ni Caren Mayenga (10), Niliam Limbu (12) na Catherine Paul (10), wote wasioona waliokuwa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Buhangija, Manispaa ya Shinyanga.

Mjema alitangaza hatua hiyo jana mkoani hapa wakati wa kuaga miili ya wanafunzi hao katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, huku akiwataka wasimamizi wa wanafunzi wawe waangalizi wa watoto ili hata linapotokea tatizo, wasaidiwe kwa wakati.

"Rai yangu kwa shule zote za mabweni, waweke ulinzi pamoja na kutoa elimu ya kuzima moto kwa shule hizo ili matukio kama hayo yasiwe yanatokea kwenye shule mbalimbali za bweni," aliagiza Mjema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi akizungumzia tukio hilo, alisema moto huo ulianza kuwaka juzi majira ya saa tano usiku wakati wanafunzi hao wakiwa wamelala.

Kamanda Magomi alibainisha kuwa kati ya wanafunzi 32 waliokuwa ndani ya bweni hilo, 29 waliokolewa na watatu walifariki dunia. Alisema wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Buhangija, Fatuma Khamis aliwashukuru wananchi waliojitokeza kusaidia kuzima moto huo, akibainisha kuwa wanafunzi waliokuwamo kwenye bweni hilo ni wasichana 32, wakijumuisha wasioona 11, wenye ulemavu wa kusikia watatu na wenye ualbino 18.

Alisema kituo kina wanafunzi 163 wakiwamo wenye ualbino 77 (wavulana 39 na wasichana 38); wasioona 20 (wavulana tisa na wasichana 11) na wenye ulemavu wa kusikia viziwi 66 (wavulana 31 na wasichana 35).

"Kwa masikitiko makubwa tumepoteza wanafunzi watatu waliofariki dunia na bweni limeteketea kwa moto, kwa kweli hii ni ajali iliyoacha simanzi kwetu," alisema Khamis.

# Wahitimu waaswa kuhusu maadili

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael, amesema kwa sasa taifa linakabiliwa na changamoto ya uvunjifu wa maadili hususan kwa vijana.

Dk. Michael aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa mahafali ya 17 ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) huku akiwataka wahitimu kuwa raia wema na kuendeleza maadili na uzalendo kwa mustakabali wa taifa.

Katika mahafali hayo, wanafunzi 5,480 walihitimu mafunzo yao kwa mwaka wa masomo 2021/22 na kati yao, wanawake ni asilimia 55.1 na wanaume ni asilimia 44.9.

"Ni wazi kuwa maadili ya sasa hususan kwa vijana yameporomoka. Wahitimu mnaomaliza mkawe chachu ya kuwa mfano wa kuigwa kwa wengine ili taifa liwe na vijana wenye maadili," alisema.

Dk. Michael alisema kama ilivyo dira ya chuo kuwa kitovu cha utoaji maarifa kwa wahitimu, aliwataka wakatumie maarifa kukitangaza kwa mazuri.

Alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa uongozi wa chuo ili kuhakikisha changamoto zinazokikabili zinamalizika.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema chuo kina matatizo makuu mawili ikiwamo la ufinyu wa bajeti na upungufu wa wafanyakazi katika idara za uendeshaji na taaluma ikilinganishwa na uhitaji.

Alisema wameanzisha miradi mbalimbali ambayo imekuwa ikiigharamia kupitia asilimia 40 ya mapato yake ya ndani lakini kiasi cha fedha kinachohitajika ni kikubwa hivyo imekuwa ikikwama na kuiomba serikali iwashike mkono ili kuifanikisha.

Prof. Mwakalila alisema chuo hicho kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 6 ya mwaka 2005 na chimbuko lake ni kilichokuwa Chuo cha Chama Kivukoni ambacho kilianzishwa rasmi Julai 29, mwaka 1961.

Alitaja dira ya chuo ni kuwa kitovu cha utoaji wa maarifa bora kwa kutoa elimu na mafunzo kuhusu ubunifu na uvumbuzi.

Alisema majukumu mengine ni kuendesha mafunzo ya elimu ya kujiendeleza, kufanya utafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu katika sekta ya umma na sekta binafsi sambamba na huduma kwa jamii.

Alisema chuo kimekuwa na mafanikio ikiwapo ongezeko kubwa la udahili sambamba na miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utitiri wa mapambano ya ngumi usikiuke sheria

**KATIKA** siku za hivi karibuni kumeibuka wimbi la uwepo wa mapambano ya ngumi yanayoandaliwa kwenye mikoa mbalimbali hapa nchini.

Ngumi ni moja ya michezo ambayo imewahi kuitangaza vyema Tanzania, kuliletea taifa sifa na heshima kwa nyakati tofauti.

Mabondia wa Tanzania walifanya vizuri katika mapambano ya kimataifa wakiwa hapa nyumbani au kwenye ardhi ya ugenini, lakini waliibuka mashujaa kwa kushinda mikanda ambayo walikuwa wakiiwania kwenye mashindano husika.

Miaka ya nyuma Tanzania ilishuhudia mabondia wake kama Rashid Matumla 'Snake Boy' akishinda mikanda mbalimbali ya kimataifa na katika siku za hivi karibuni, Hassan Mwakinyo, naye alianza kuipeperusha vyema bendera ya taifa (kabla ya sintofahamu iliyojitokeza hivi karibuni huko alipokuwa Uingereza) na kuanza kuwavutia mapromota kuandaa mapambano.

Mbali na kuwavutia waandaaji hao, lakini pia imeonekana kama sehemu ya kuhamasisha mabondia chipukizi kuupenda mchezo huo, na kurejesha nguvu katika kujiandaa kwa ajili ya kupambana kuanzia ngazi ya riadha na baadaye kuhamia kwenye ngumi za kulipwa.

Baada ya kuona na kubaini mchezo huo ulipoteza umaarufu wake, mapromota kutoka sehemu mbalimbali wameamua kuwekeza ili kuufanya urejee kwenye kasi na nafasi iliyowahi kuushika lakini ikiwapa mabondia heshima pamoja na taifa lao pendwa.

Hakuna ubishi mapambano hayo mbali na kutoa burudani kwa wananchi, lakini pia huwasaidia kiuchumi mabondia na wote wanaoshiriki kwa namna moja au nyingine kwenye uandaaji, kwa maana halisi husaidia kutengeneza ajira kwa kada mbalimbali.

Inafahamika lengo kuu la kuandaa mapambano hayo ni kuwatangaza wachezaji hao, kuwapa mazoezi sahihi kuelekea mashindano ya kimataifa yaliyoko mbele yao lakini kuwaongezea kipato kupitia ada wanazolipwa kwa makubaliano rasmi kabla ya kupanda ulingoni, lakini katika siku za hivi karibuni tumeshuhudia baadhi ya mabondia wakipanda ulingoni mara kwa mara.

Ili kuulinda mchezo husika, ni vyema wasimamizi wa mchezo huo wakahakikisha kanuni, sheria na taratibu hazikiukwi na kwa kufanya hivyo, itawasaidia mabondia kulinda vipaji pamoja na afya zao, badala ya kuweka mbele maslahi ya leo.

Endapo wasimamizi watakaa kimya na kuruhusu mabondia au bondia kuonekana anavunja sheria kwa sababu ya 'njaa' yake binafsi au kwa ushawiki wa promota, jambo hilo lisiachwe liendelea kutoka kwa afya ya maendeleo ya mchezo huo wa ngumi.


Kwa sasa kuna mabondia ambao wameshakuwa maarufu na hawako tayari kuona wanapanda ulingoni mara kwa mara kwa sababu wanafuata kanuni, lakini wapo mabondia chipukizi ambao hawana umaarufu, nao pia wanatakiwa kulindwa kwa kutopata vibali vya kupanda ulingoni nje ya muda sahihi unaotakiwa kutoka pambano moja hadi pambano linalofuata.

Haitakuwa busara pia kuacha kuwapongeza wadhamini na mapromota ambao wanajitokeza kuandaa mapambano mbalimbali kwa sababu wamesaidia kuongeza hamasa katika mchezo huo ambao miaka mitano iliyopita ulionekana kufifia hapa nchini.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imekuwa ikisisitiza kila idara kutimiza majukumu yake ipasavyo, hivyo kuheshimu taratibu ni moja ya mwongozo ambao serikali kupitia wizara hiyo imesema kwa ajili ya kuhitaji kupata matokeo chanya kwa wanamichezo wake katika kila mashindano watakayoshiriki.

Tunaamini kila mtu atakapofanya majukumu yake kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu, basi malengo yaliyodhamiriwa ya kuuendeleza mchezo wa ngumi yatafikiwa na hatimaye kupata vipaji vipya vitakavyoiletea nchi medali mbalimbali na si kupigana kwa lengo la kunufaisha mapromota au kumaliza tatizo la leo la bondia husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Simba, Yanga wasinyimwe uhuru kutoa mawazo

**TUNAJUA** kwa sasa wanachama wa klabu za Simba na Yanga hawana tena mamlaka ya kuamua mustakabali wa klabu zao kama ilivyokuwa zamani.

Tunakumbuka wakati ule wanachama wakiona mambo hayaendi vizuri, wanaitisha mkutano na kuamua kile ambacho wataona ni muhimu kwa manufaa ya klabu zao kwa wakati huo.

Ndiyo wakati tuliona mapinduzi makubwa ya viongozi. Timu ikifungwa, kesho yake tu wanachama wanaitisha mkutano, kama hawawataki viongozi wanapitisha maazimio ya kuondoa uongozi.

Baadaye nakumbuka Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) liliingilia kati na kutengeneza katiba kuzipeleka kwa wanachama wake kuweka utaratibu wa kuwaondoa viongozi na si kiholela kama ilivyokuwa ikifanyika.

Tukaanza kuona sasa angalau viongozi wa klabu hizi wakikaa mpaka vipindi vyao vinamalizika, ingawa bado walikuwa wakiongoza kwa matatizo makubwa. Nia yangu si kuunga mkono yale ambayo yalikuwa yakifanywa na wanachama wa kipindi hicho la hasha kwa sababu kuna wakati pia baadhi yao walikuwa wakihongwa na baadhi ya watu walio nje ya madaraka kufanya vurugu ili kuuondoa uongozi na wao waingie.

Ni kutaka kuonyesha jinsi wanachama walivyokuwa na nguvu ya moja kwa moja ya kuwawajibisha viongozi wao, walikuwa na nguvu kuliko viongozi waliowaweka madarakani. Kwa sasa haipo hivyo. Mpira umebadilika. Mpira kwa sasa ni biashara ambapo inahitaji wawekezaji. Hakuna mwekezaji ambaye anaweza kuwekeza halafu bado eti wanachama wakaendelea kuwa na nguvu ya kufanya maamuzi. Dunia nzima kwa sasa mwekezaji ambaye anatengeneza watu wake anawaamini kwenye bodi kwa kushirikiana na wale wa upande wa wanachama, au mfumo wowote ule wa uendeshaji wa soka la kisasa, watu wachache ndiyo wenye maamuzi.

Bodi ndiyo inawawakilisha wanachama wote, na ndiyo wanaoiendesha klabu. Aina hii ya uongozi wa soka la kisasa la wawekezaji limewanyang'anya wanachama maamuzi juu ya klabu zao. Binafsi wala sipingi kwa sababu kwa sasa lipo huko. Mwenye pesa ndiye anayeamua nini kifanyike.

Mimi nina wasiwasi pia inaonekana pia wanachama wanataka kupokwa hata haki yao waliyobaki nayo ya kutoa maoni yawe hasi au chanya juu ya klabu zao pendwa.

Nimemsikia kiongozi mmoja wa tawi moja la Yanga akiwapiga mkwara wanachama wanaopenda kuongea na Waandishi wa Habari mara baada ya mechi zao. Akaenda mbali zaidi kwa kutangaza kuwa watamsimamisha mwanachama wao mmoja kwa kosa hilo. Kisa eti alitoa maoni yake, na wengine wanawasema viongozi wao.

Akawapiga marufuku wanachama kuongea na waandishi. Hili halikubaliki hata kidogo. Wanachama wamenyang'anywa maamuzi kwenye klabu yao, sasa inataka kwenda mbali zaidi kutaka kuwapoka hata ile haki waliyobakia nayo ya kutoa maoni yao. Huu sasa hauwezi kuuzungumzia vingine zaidi ya udikteta. Iwe kwa Yanga au Simba viongozi waachane kabisa na jambo hili.

Tumeona hivi karibuni Simba haifanyi vema kwenye michezo ya ligi, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wamekuwa wakiwaonyeshea vidole vya shahada viongozi wao na wachezaji pia. Iwapo atatokea kiongozi yoyote wa Simba wa juu au matawi akawakataza wasiongee, litaendelea kuwa tatizo kubwa kwenye soka la Tanzania.

Hakuna kiongozi anayeweza kujitathmini, kuona anafanya vema au anakosea kama hataki watu waongee.

Halafu asili ya mchezo wa soka ni kuongea. Iwe kuongea kwa kufurahi, kulalamika, au kutoa maoni hata kama ataongea vibaya au jambo ambalo halipendezi. Hii ni haki ya kwanza ya binadamu anayopewa na Mwenyezi Mungu, haki ya kujieleza na hata kwenye Katiba ya Tanzania imebainishwa bayana kuwa wananchi wanayo haki hiyo.

# Kituo cha taarifa za ardhi kujengwa

**Na Anthony Ishengoma,** DODOMA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, jana alipokea hati ya makubaliano kutoka ujumbe wa serikali ya Korea ya Kusini kuhusu mradi wa uanzishwaji wa kituo cha mafunzo ya taarifa za kijiografia na usimamizi wa ardhi.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. Bilioni tano utatoa mafunzo hayo kupitia kampuni ya Lx Consortium ya Korea Kusini na utaanza hivi karibuni jijini hapa baada ya kuzinduliwa na serikali za Tanzania na Korea Kusini baada ya maandalizi kukamilika.

Akizungumza na wajumbe wa menejimenti ya Wizara ya Ardhi, Dk. Kijazi aliwataka watendaji wa wizara kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufanikisha mradi huo. Alisema mradi huo ni wa aina yake barani Afrika kwa kuwa ni mpya katika nchi za Afrika.


"Tukifanikisha mradi huu kwangu mimi ni ushindi mkubwa na utakuwa wa mfano kwa nchi za Afrika. Nawaagiza kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa kufanikishwa mradi huu ambao utakuwa wa aina yake nchini na Afrika kwa ujumla," alisema.

Dk. Kijazi alitumia fursa hiyo kuwapongeza baadhi ya watumishi wa wizara ambao wameanza kunufaika na mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uwezo kuhusu taarifa za kijiografia na utawala wa ardhi ambayo yametolewa na LX Consortium kwa njia ya mtandao.

Utekelezaji wa mradi huo mkubwa unakuja kutokana na kutiwa saini hivi karibuni kwa hati ya makubaliano kati ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula na yule wa Ardhi, Miundombinu na Usafirishaji wa Korea Kusini, Won Hee-ryong, Seoul, Korea Kusini, kupitia hati ya makubaliano (MOU) ya ushirikiano kwenye sekta ya ardhi na menejimenti ya taarifa za kijiografia.

Makubaliano ya nchi hizo mbili yanalenga kuweka mazingira rafiki kwa Watanzania kupata utaalam na uzoefu kwenye nyanja za upimaji na ramani kupitia mipango na miradi ya mafunzo ya kuendeleza rasilimali watu kwa maendeleo endelevu ya sekta ya ardhi na kuwapo kwa fursa zaidi kwa Watanzania kupata mafunzo ya muda mrefu nchini Korea.

Kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu kutaimarisha ushirikiano uliopo kati ya Wizara ya Ardhi ya Tanzania na ile ya Korea Kusini katika kukuza matumizi ya teknolojia za kisasa kwenye sekta ya ardhi ili kuboresha utoaji huduma katika fani zote za utawala wa ardhi na kutimiza azma ya serikali ya kusajili ardhi yote nchini.




Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Chande (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Ofisa wa Vodacom M-Pesa, Filbert Mushi (kushoto), kuhusu namna kampuni hiyo ilivyokuwa mstari wa mbele kutoa huduma bora za fedha kidijitali kupitia M-Pesa na kuisaidia serikali katika ajenda yake ya kuhakikisha Tanzania inaingia katika ulimwengu wa kidijitali, alipotembelea maonyesho ya wiki ya huduma za kifedha yanayoendelea jijini Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIRA yabanwa wanaopata majanga kutolipwa stahiki

**Na Farida Ramadhani,** MWANZA

SERIKALI imeiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) kuzichukulia hatua za kisheria ikiwamo kuzifutia leseni za kufanyabiashara, kampuni zinazoshindwa kuwalipa fidia wateja waliopata majanga.

Maagizo hayo yalitolewa jana na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande alipotembelea na kukagua mabanda ya maonyesho katika maadhimisho ya pili ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yanayoendelea katika viwanja vya Rock City Mall jijini Mwanza.

Alisema waathirika wamekuwa wakipata usumbufu wakati wa kudai fidia kwa kuwa hawalipwi kwa wakati na hata ukifika muda wanapolipwa fedha inakuwa imeshashuka thamani.

"Malalamiko mengi yamekuja wizarani kuhusu kampuni hizi za bima, ninaiagiza TIRA izichukulie hatua zile ambazo hazifuati sheria na taratibu," aliagiza Chande.

Pia aliitaka Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima kutoa suluhu kwa wakati na kwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali ya nchi na kuhakikisha kuwa kampuni za bima zinawajibika ipasavyo kwa matendo yake ili wahusika kupata haki zao kwa wakati.

Naibu waziri huyo pia aliiagiza Benki Kuu (BoT) kukutana na benki na taasisi za fedha mbalimbali nchini kutafuta suluhu ya kupunguza riba za mikopo ili wananchi wengi wanufaike na kujikwamua kiuchumi.

Chande alifafanua kuwa serikali imeshusha riba ya mikopo inayokopwa na taasisi hizo hadi asilimia tatu, lakini kiwango cha riba cha kuanzia asilimia tisa kwenda juu kinachotozwa na taasisi za fedha kwa wakopaji ni kikubwa kwa wananchi wa kipato cha chini.

Akizungumzia masoko ya mitaji na dhamana, Chande aliiagiza Mamlaka ya Soko la Dhamana na Mitaji (CMSA) kuongeza wigo wa elimu kwa umma kuhusu dhamana hizo na namna mwananchi anavyoweza kunufaika kwa kuwa uelewa ni mdogo.

Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha nchini kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja, alisema maadhimisho hayo hayatoi elimu pekee bali ni fursa adhimu kwa ajili ya kuchukua maoni na ushauri wa wananchi kuhusu maeneo mbalimbali ya huduma za fedha yanayotakiwa kuboreshwa.

Alisema maoni yaliyotolewa yamechukuliwa na yatafanyiwa kazi katika masuala ya kisera, taratibu na kutekelezaji ili kuhakikisha sekta ya fedha inakua kwa asilimia 80 ya Watanzania kupatiwa elimu ya fedha ifikapo 2025.

# Chama chapata bilioni 3.4/- kuanzisha kiwanda mafuta

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU) kimepokea mkopo wa Sh. bilioni 3.4 kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kukamua mafuta ya mbegu za Pamba ili kuongeza thamani ya mazao ya wakulima na uchumi wa kaya.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hamisi Majohoro, aliyabainisha hayo jana ofisini wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu msimamo wa chama kutokana na kauli iliyotolewa na aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Bashiru Ally, akiwa mkoani Morogoro kuhusu wakulima na pembejeo.

Alisema mkopo wa ujenzi wa kiwanda hicho umetolewa na serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Alisema kiwanda hicho kitaongeza uzalishaji wa pamba katika misimu ijayo na kupunguza tatizo la uhaba wa mafuta ya kula kwa wananchi hususani wa Kanda ya Ziwa na ujenzi. Pia alisema msimu huu wakulima wanatarajia kuzalisha kilo milioni sita za pamba kulinganisha na msimu uliopita, walipoweka malengo ya kuzalisha kilo milioni 3.5 lakini uzalishaji halisi ulikuwa kilo milioni 2.189 huku Kahama ikizalisha kilo milioni 1.759 pekee.

Kadhalika alisema chama kimeongoza ushindani wa soko na kampuni zingine zinazonunua zao hilo kwa sababu msimu uliopita walinunua kilo moja kwa Sh. 1,600 bei ya awali hadi 2,020 na zaidi ya Sh. bilioni 3.363 zilitumika kununua pamba, hivyo malighafi ya kuanzia kuchakata mafuta ipo.

Majogoro alisema kwa kipindi cha miaka minne mfululizo chama hicho kimeaminiwa na serikali na kupewa dhamana ya kuagiza pembejeo na viuatilifu vya pamba na kuvisambaza kwa wakulima nchi nzima na msimu huu wameagiza viuatilifu vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 150.

"Mwaka 2017 hadi 2020 bei ya pamba ilikuwa 850 mpaka 1,100 kwa kilo moja, lakini sasa imepanda hadi 2,020 kwa kilo na hii ndiyo sababu inayotufanya kujenga kiwanda cha kukamua mafuta yatokanayo na mbegu za zao hili ili kuongeza thamani mazao ya wakulima na kupata kipato," alisema Majogoro.

Mmoja wa wakulima wa kata ya Bukomela, Halmashauri ya Ushetu, Kulwa Shoto, alisema kiwanda kitakapokamilika, kitaongeza ushindani wa soko la zao hilo na kampuni zingine, hivyo wakulima watapata fedha za kukidhi mahitaji yao na kuondokana na bei ya Sh. 850 iliyokuwa ikiwaumiza wakulima.

Hivi karibuni, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ilitoa pembejeo bure kwa vijana 71 kutoka kata 12 wenye uwezo wa kulima ekari tano na kuendelea, zenye thamani ya Sh. milioni 66.8 kutoka mapato ya ndani na kupitia mkopo huo, ekari 415 za mahindi, mpunga, alizeti na pamba zitalimwa.

# Wanafunzi 960 waacha shule

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAFUNZI 963 wa shule za sekondari mkoani Njombe hawajafanya mtihani wa kidato cha pili kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utoro.

Imebainishwa kuwa kati yao, wavulana ni 584 na wasichana 379 na kwamba idadi yao ni sawa na asilimia sita ya walioandikishwa kufanya mtihani huo mwaka huu.

Akizungumza katika kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa (RCC) jana, Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Nelasi Mulungu alisema wanafunzi hao walianza kidato cha kwanza vizuri lakini walipoingia kidato cha pili, wakaacha shule.

"Wanafunzi waliofanya mtihani mwaka 2022 waliandikishwa shule ya sekondari mwaka 2021, kidato cha kwanza wakiwa jumla ya wanafunzi 15,256. Kati yao, wavulana 6,664 na wasichana 8,546, hivyo walistahili kufanya mtihani wa kidato cha pili mwaka 2022," alisema.

Mulungu alibainisha kuwa wanafunzi watoro wengi wao ni wavulana ambao inadaiwa huwa wanakwenda kufanya vibarua mikoa jirani.

"Tumewajulisha mamlaka za halmashauri na wakuu wa wilaya kuwatafuta ili kuwarudisha shuleni, kwa sababu Rais Samia alitoa ridhaa kwa watoto wote ambao wameacha shule kwa sababu mbalimbali warudi shuleni, awe wa sekondari awe wa shule za msingi. Kwa hiyo, mamlaka husika zinaendelea kuwatafuta," alisema Mulungu.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Njombe, Subilaga Mwaigwisya alisema tatizo hilo linachangiwa na wazazi kuwaachia majukumu ya familia watoto wa kiume.

"Tumekuwa na ugomvi mkubwa na familia, wazazi hasa kwa watoto wa kiume baada ya baba kuondoka yule mtoto wa kiume anachukua yake au wakati mwingine anakwenda kufanya shughuli za kiuchumi, kwenye kubeba mbao na biashara ndogo," alisema Mwaigwisya.

Hata hivyo, ofisa huyo alishindwa kubainisha waliko wanafunzi wa kike ambao ni watoro hasa kwa kuzingatia mkoa huo hauna ndoa za utotoni.




Baadhi ya wanawake wa kata ya Lubugu, Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, wakichota maji safi na salama katika moja kati ya vituo 30 vya maji vilivyo katika mradi wa Nsolabubinza, unaotoa huduma hiyo kwa vijiji vitatu vya kata hiyo, uliojengwa chini ya miradi ya Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani humo juzi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Vijiji vitano vyaagana na kilio cha uhaba wa maji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ZAIDI ya watu 30,000 kutoka katika vijiji vitano vya Nsola, Kisamba, Bubinza, Yichobela na Izizimba 'B' wilayani Magu na Kwimba mkoani Mwanza, wameanza kunufaika na miradi ya maji iliyotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mwaka 2021/22 na kugharimu Sh. bilioni tatu.

Wakifafanua kuhusu miradi hiyo kwa nyakati tofauti, Meneja wa RUWASA wilayani Magu, Daud Amlima na Meneja wa RUWASA wilayani Kwimba, Godliver Gwambasa walisema kuwa ndani ya wilaya hizo wanayo miradi yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni tatu ambayo tayari imetekelezwa kwa asilimia 100 kupitia fedha za kukabiliana na athari za UVIKO-19.

"Kwa wilaya yetu ya Magu ni miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 1.5 ambayo imekamilika na inatoa maji safi na salama kwa wananchi zaidi ya 20,000 kutoka katika vijiji vinne ndani ya kata mbili, wananchi wanachangia Sh. 30 kwa ndoo moja ya lita 20, wateja wa majumbani wanalipia Sh. 1,500 kwa uniti moja," Amlima.

Alibainisha wamejenga matangi matatu ya Nsola yenye uwezo wa kuhifadhi lita 90,000 na tangi la Bubinza lenye uwezo wa kuhifadhi lita 135,000 na Yichobela lenye uwezo wa kutunza lita 75,000.

"Kwa sasa tumekamilisha miradi ya maji ambayo inatoa huduma kwa wananchi zaidi ya 10,000 na tunayo miradi mingine tunatekeleza yenye thamani ya zaidi Sh. bilioni 18 inayotarajiwa kuhudumia wananchi zaidi ya 35,000 na ikikamilika itakuwa imemaliza tatizo la maji katika vijiji vya Wilaya ya Kwimba kwa asilimia mia moja kumtua mama ndoo kichwani," alisema Gwambasa.

Wanufaika wa miradi hiyo walielezea katika maeneo tofauti kuvutiwa na upatikanaji wa huduma hiyo kwa kuwa imetatua tatizo la uhaba wa maji lililokuwa linawakabili.

"Ili kupata maji tulikuwa tunalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa sita kwenda ziwani na kuna vipindi tofauti wenzetu walivamiwa na hata kuliwa na mamba walipokwenda ziwani kuchota maji alfajiri," alisifu Elizabeth Sahani, mkazi wa Bubinza.

Wase Zabron, mkazi wa Kijiji cha Kisamba, alisema: "Muda mwingine tulilazimika kuamka usiku kwenda kuchota maji ili ikifika asubuhi tupate nafasi ya kufanya shughuli zetu nyingine za kilimo na kuna vipindi waume zetu hawakuamini mienendo yetu".

Diwani wa Lubugu, Lucas Zablon alipongeza kutekelezwa kwa miradi hiyo iliyokuwa imesimama kwa miaka 15 kutokana na ukosefu wa fedha.

# Wahitimu Chuo cha Kodi wapewa jukumu utatuzi kero za kodi

**Na Halfani Chusi**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, amewataka wahitimu wa Chuo cha Kodi kuisaidia serikali kujibu hoja zinazohusiana na vikwazo vilivyopo katika eneo hilo ili kuboresha mfumo wa ukusanyaji kodi.

Lawrance Mafuru alitoa rai hiyo jana wakati wa mahafali ya 15 ya chuo hicho mkoani Dar es Salaam, akitunuku vyeti kwa wahitimu 489.

Alisema ulipaji wa kodi ni muhimu katika ustawi wa nchi, hivyo wanafunzi waliohitimu, hawana budi kuwa mabalozi wazuri katika jamii na serikali katika kutatua vikwazo.

"Chuo cha Kodi katika nchi yetu kina wajibu wa kipekee kutoa wataalamu ambao wataisaidia serikali katika kufanya utafiti ili kuleta njia sahihi ya ulipaji kodi, lakini utafiti huo ujikite katika kujibu hoja, pamoja na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

"Njia ya kujiokoa na mikopo katika nchi yetu ni pamoja na sisi wenyewe kuweka mipango thabiti na wezeshi katika kukusanya mapato ya ndani. Taasisi hii inaweza kwa sababu imejikita katika kutoa elimu bora tangu ilipoanzishwa," alisema.

Aliiagiza Mamlaka ya Mapato (TRA) kukisaidia chuo hicho kwa kuwezesha kupata wataalamu wengi wenye taaluma ya kutosha ili kutoa elimu hiyo kwa wanafunzi.

"Tukiwa na watu wengi wenye taaluma na wanaoujua umuhimu wa kulipa kodi, kutaipunguzia kazi serikali na mamlaka inayohusika katika shughuli nzima ya ukusanyaji wa mapato.

"TRA endeleeni kutoa huduma na ushauri, serikali itaendelea kuweka sera na mazingira rafiki katika ukusanyaji wa kodi. Kwa hiyo mna jukumu la kukisimamia chuo hiki," alisisitiza.

Aliwataka wahitimu hao kutojihusisha na vitendo viovu akiwasihi kutumia taaluma waliyoipata kuleta matokeo chanya katika jamii.

"Kumaliza chuo isiwe mwanzo wa kuanza kufanya vitendo ambavyo havileti sifa nzuri, nimesikia utaratibu wa chuo hiki hata kama umehitimu lakini usipokuwa na sifa nzuri kwa jamii unaweza kufutiwa matokeo na cheti chako.

"Kwa hiyo, niwaombe sana mkawe watii, mkaisaidie jamii pamoja na kuendelea kutoa elimu ili tupate kizazi kitakachokuwa kinaelewa nini umuhimu wa kodi kwa taifa letu," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Isaya Jairo aliwataka wahitimu kwenda kusaidia jamii, akibainisha jumla yao ni 489. Kati yao, wanaume 291 na wanawake 198 na wamehitimu katika ngazi za cheti cha Uwakala wa Forodha cha Afrika Mashariki (CFFPC), cheti cha Awali cha Usimamizi wa Forodha na Kodi (CCTM), Stashahada ya Usimamizi wa Forodha na Kodi (BCTM) na Stashahada ya Uzamili katika Kodi (PGDT).

Vilevile, aliongeza kuwa chuo hicho kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa watu 271 wakiwamo watumishi wa TRA na wadau wengine kuhusu umuhimu na ukusanyaji wa kodi.

Mmoja wa wahitimu wa chuo hicho aliyefanya vizuri katika fani ya Usimamizi wa Forodha na Kodi, Edwini Norasco, alisema siri ya mafanikioa yake ni kumtanguliza Mungu na kusoma kwa bidiii

"Nimepata zawadi nyingi siku ya leo, kuwa ndiye mwanafunzi aliyefanya vizuri zaidi lakini siri kubwa ilikuwa ni kumtanguliza Mungu na kusoma kwa bidii.

"Pia chuo kina mazingira rafiki kwa mwanafunzi kusoma na walimu wazuri, lakini wanafunzi wote tuliohitimu leo (jana) tulikuwa vizuri licha ya wengine kutopata zawadi," alisema.

Kinara mwingine katika fani ya Shahada ya Kodi, Glory Same, alisema pengo kubwa analoliona ni uelewa mdogo kwa wafanyabiashara na wadau wengine wa maendeleo juu ya kodi.

"Watu wakishapata uelewa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi, wakijua kwanini wanalipa kodi, hawataisumbua serikali kwa sababu watakuwa wanajua

# TGDC yajitosa kukabili upungufu umeme nchini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMPUNI ya Uendelezaji Joto Ardhi nchini (TGDC) imesema wakati wowote kuanzia sasa itaanza rasmi utekelezaji wa miradi mitano ya rasilimali joto ardhi katika mikoa 16 kwa ajili ya kukabiliana na makali ya mgawo wa umeme.

TGDC ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme (TANESCO) ambayo inachimba na kuzalisha nishati ya joto ardhi inayochimbwa urefu wa kilometa tatu kwenda chini, ikiwa na uwezo wa kuzalisha megawati 5,000.

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Shakiru Kajugus, akizungumzia mpango huo jijini Arusha jana, alisema nishati hiyo ya joto ardhi inapatikana kwa wingi katika maeneo yanayopitiwa na Bonde la Ufa.

"Kwa sasa tuko katika hatua ya utafiti pale Ziwa Natron, kabla ya kuanza utekelezaji wa uzalishaji wa umeme kupitia joto ardhi. Mradi huo utakapoanza utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 60 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2025," alisema.

Kwa mujibu wa Kajugus, katika utafiti wao wamegundua kuwapo viashiria vya rasilimali adimu ya joto ardhi katika Ziwa Natron lililoko Wilaya ya Ngorongoro na Ziwa Manyara lililoko mkoani Arusha. "Mradi huu wa Ziwa Natron kwa kuanzia tutazalisha megawati 10, baada ya hapo tunaendelea na upanuzi zaidi. Ili kuukamilisha na kuanza kutoa huduma mradi huu umetengewa zaidi ya Sh. bilioni moja. Tunaamini mradi huu utaleta manufaa makubwa kwa wananchi kwa kuwa ni nishati endelevu ya kisasa isiyotegemea mabadiliko ya tabianchi," alisema Kajugus.

Kwa sasa mradi huo kwa Tanzania umetekelezwa katika maeneo matano, ikiwamo Ngozi na Mbaka-Kiejo zilizoko Rungwe, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Songwe na Pwani, ambako miradi hiyo iko kwenye hatua ya uhakiki kwa ajili ya kuchimba visima.

Eneo lingine ni katika Ziwa Natron lililoko Mkoa wa Arusha, ambako watafiti wanaendelea na utafiti za kisayansi ambazo zinatarajiwa kumalizika mwaka 2023.

Mwenyekiti wa Bodi ya TGDC, Prof. Shubi Kaijage, akizungumzia mradi huo, alisema nishati hiyo inapatikana chini ya ardhi kwa kutumia joto lililopo chini ya ardhi na utakapokamilika utapunguza tatizo la makali ya mgawo wa umeme uliopo nchini kwa sasa. "Sisi kama bodi tunaendelea kuhakikisha tunasimamia kikamilifu mradi huu ili ukamilike kwa wakati na tunaomba kampuni hii iendelee kutekeleza majukumu yake ili tuendelee kupata vyanzo zaidi vya umeme," alisema Prof. Kaijage.

Kaimu Meneja Huduma za Jiosayansi, Albano Mahecha alisema viashiria vya joto ardhi vimekuwa vikipatikana katika mwendelezo wa Bonde la Ufa la Afrika Mashariki kutokana na kuwapo maeneo ya volkano na mipasuko mikubwa ya dunia.

Mahecha alisema mradi huo ambao uko ndani ya Ziwa Manyara linalohifadhiwa na Hifadhi ya Taifa ya Manyara utaongeza thamani katika eneo la utalii kwa kuwa Kenya wanatumia kwa wingi nishati hiyo ya joto ardhi inayopatikana ndani ya hifadhi.

# Bashe: Hakuna wilaya itakayokosa chakula

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amewatoa hofu Watanzania kuhusu tishio la njaa na mfumuko wa bei ya mahindi nchini, akisema hakuna wilaya itakayokosa mahindi yanayosambazwa na serikali na kuuzwa kwa bei nafuu kwa kuwa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) ina akiba ya kutosha.

Akiwa wilayani Babati jana, Bashe alisema Tanzania haina njaa kama inavyoelezwa mitaani na watu wasiolitakia mema taifa, akisisitiza kuwa kilichopanda ni bei ya mahindi. "Hayo mahindi yamepanda bei ghafla kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan ameruhusu wakulima wauze nje ya nchi mazao yao ili mkulima apate faida kubwa baada ya kutumia jasho lake kuzalisha kwa wingi," alisema.

Bashe alisema ili kuhakikisha wananchi hawapati shida ya kutafuta mahindi hayo, serikali inakusudia kutenga vituo vya kuwauzia mahindi wananchi kwa bei nafuu. Kwa mujibu wa waziri huyo, kilogramu moja ya mahindi itakuwa inauzwa kwa Sh. 700 hadi 800 na debe moja litakuwa linauzwa Sh. 14,000.

Alisema kwa kuwa kilimo ni biashara, ni vyema wananchi waelewe kuwa serikali haitamaliza vikwazo vya kilimo kwa kumtisha Rais badala yake wanatakiwa kumuunga mkono.

Waziri Bashe alisema hatua zilizochukuliwa kwa sasa na Rais Samia za kupambana na upungufu wa chakula nchini na kuzalisha kwa tija, ni kuitengea Wizara ya Kilimo bajeti ya kimkakati na matokeo yake yataanza kuonekana baada ya miaka mitatu.

Bashe alisema katika kuthibitisha jitihada hizo za Rais Samia, serikali mpaka sasa imeshatumia Sh. bilioni 180 kusambaza mbolea mikoa yote na wilaya zote.

Juzi Rais Samia akiwa katika ziarani mkoani Manyara, alizindua mradi wa vihenge na maghala ya mazao ya chakula yaliyojengwa wilayani Babati.

Vihenge hivyo vimejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 19.359, mradi huo ukilenga kuhifadhi tani 40,000 za mazao ya chakula.

Kwa sasa uwezo wa NFRA kukidhi mahitaji ya dharura ya chakula kwa miezi mitatu ni zaidi ya tani 500,000 kulinganisha na tani 150,000 zilizokuwa zinahitajika miaka ya 1992 wakala ulipoanzishwa.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Manyara, Kiria Laizer (kulia), akikabidhi cheti cha kuhitimu darasa la saba kwa mwanafunzi wa shule ya awali na msingi Blue Tanzanite ya mji mdogo wa Mirerani, wakati wa mahafali yaliyofanyika juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wizara yapongeza kuridhiwa mfumo ulinganifu elimu ufundi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Calyone Nombo amesema uamuzi wa nchi za Tanzania, Kenya na Ethiopia kuridhia kwa pamoja kutumia mfumo wa sifa wa ulinganifu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET), ni hatua muhimu kwa kuwa umeongeza kozi za mafunzo ya ufundi kutoka 44 hadi kufikia 235.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akifungua mkutano wa kikanda wa ushauri wa kiufundi wa Mradi wa Kujenga Ujuzi kwa Maendeleo na Ulingano wa Kikanda (EASTRIP), Nombo alisema mfumo huo tayari umeonyesha matokeo chanya tangu uliporidhiwa na makatibu wakuu wa wizara husika katika mataifa hayo. Alisema nchi hizo zitahakikisha kunakuwapo utekelezaji mzuri wa mradi na mifumo ya kikanda, ambayo imetengenezwa kwa pamoja ili kufikia malengo ya mradi huo wa kujenga ujuzi kwa maendeleo na ulingano wa kikanda.

"Kupitishwa kwa mfumo wa sifa za ulinganifu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET) wa kikanda na makatibu wakuu kutoka nchi za Tanzania, Kenya na Ethiopia ni hatua muhimu sio tu kwa mradi, bali pia kwa ukanda wa Afrika Mashariki. "Mafanikio haya yataruhusu nchi hizi tatu kutambua kwa pamoja mfumo wa sifa za ulinganifu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na kuwezesha uhamasishaji wa wanafunzi na kazi katika ukanda. Hii ni hatua muhimu kuelekea kuongeza udahilii wa wanafunzi wa kikanda katika programu za muda mrefu na za muda mfupi," alisema.

Aliongeza kuwa mfumo huo utachangia kusukuma utekelezaji wa itifaki ya soko la pamoja la Afrika Mashariki, akielekeza taasisi za kitaifa zinazosimamia TVET na taasisi za uhakiki wa ubora, kutumia sifa za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na mfumo wa kikanda, kuhakikisha ubora unaohitajika katika kutoa mafunzo ya elimu ya ufundi unafikiwa.

Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzi ya Ufundi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Noel Mbonde alisema kupitia mradi huo, Tanzania imepata dola za Marekani milioni 75 kwa ajili ya kuanzisha vituo vinne vya umahiri katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) kwa ajili ya ndaki zake za Mwanza na Dar es Salaam.

Dk. Mbonde alisema kila chuo kimepatiwa dola za Marekani milioni 16.125, isipokuwa NIT ambao wamepatiwa dola za Marekani milioni 21.25. Alisema asilimia 80 ya fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi na asilimia 20 kwa ajili ununuzi wa mitambo na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Mkurugenzi wa DIT Ndaki ya Mwanza, Albert Mmari alisema kupitia mradi huo kuna kituo cha umahiri wa mazao ya ngozi, akipongeza mradi huo kwa kuboresha miundombinu na ujenzi ukikamilika utaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 200 hadi kufikia 2200 kwa mwaka.

# Serikali yashtukia ujenzi bila wakadiriaji majenzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imeagiza taasisi zake zote, mashirika ya umma na miradi ya majengo inayotekelezwa na serikali, isijengwe bila ya kuwahusisha wataalamu wa ukadiriaji majenzi ili kuokoa gharama zinazotumika kununua malighafi za ujenzi ambazo hazihitajiki.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alisema uamuzi wa serikali kuelekeza kutumika kwa wataalamu hao unalenga kuwatumia wataalamu hao kuhahakikisha miradi inayotekelezwa inaakisi thamani halisi ya fedha za umma.

Prof. Mbarawa aliagiza hayo jana wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa 28 wa Wakadiriaji Majenzi Tanzania (TIQS) unaoendelea jijini Arusha.

"Makandarasi wanapotekeleza miradi hiyo ya miundombinu, wanakuwa na wakadiriaji majenzi. Kwa hiyo, ni muhimu pia kwa upande wa serikali na washauri elekezi, nao wawe na wanataaluma hao ili kuhakikisha fedha za serikali zinasimamiwa ipasavyo.

"Ninawaomba muwe na ushirikiano wa kazi na kitaaluma, ikitokea miradi ya serikali, ni muhimu kampuni zenu kuungana ili kufanya kazi kwa wakati, ubora na pia kubadilishana utaalamu.

"Kwa miradi mikubwa ya serikali, bila kuungana kutafanya watu wachache zaidi washiriki katika utekelezaji wa miradi hiyo na labda kutokukamilisha kazi kwa wakati," alisema Prof. Mbarawa.

Waziri huyo pia alisema kitendo cha kuwapo washiriki kutoka nchi za Afrika Mashariki na nchi jirani katika mkutano huo ni ushirikiano mzuri, hivyo ni vyema ufanyaji kazi uwe ni wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kubadilishana ujuzi.

"Serikali inafahamu jinsi wakadiriaji majenzi wanavyofanya kazi nzuri katika halmashauri za wilaya, taasisi za uchunguzi na ukaguzi na kwenye serikali kuu kwa ujumla. Hivyo, serikali kwa ujumla wake inatambua umuhimu wa fani hii na kuithamini," alisema.

Waziri huyo pia aliagiza wakadiriaji majenzi kuzingatia mkataba wao wa ushirikiano, huku akiwahimiza kuanzisha rasmi ushirikiano wa kitaaluma kwa kuwa nchi za Afrika Mashariki zimekubaliana kushirikiana katika sekta mbalimbali.

Awali, Rais wa Taasisi ya Mkadiriaji Majenzi nchini, Bernard Ndakidemi alisema wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kukosekana Sheria ya Majengo, kutotambulika kwa fani zinazoshabihiana na fani ya ukadiriaji majenzi na kutokutambulika kuajiriwa kwa wataalamu hao serikalini pamoja na kutotumika vya kutosha kwa wakadiriaji majenzi katika kazi za miundombinu ikiwamo barabara, madaraja na miradi ya maji.



Aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Iringa (UOI), Askofu mstaafu Elinaza Sendoro (wa pili kulia), akimkaribisha Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi mstaafu, Jenerali Venance Mabeyo, baada ya kusimikwa kuwa Mkuu mpya wa Chuo hicho, katika mahafali ya 25 ya mwaka 2021-2022, chuoni hapo, jana. Kulia ni Makamu wa Mkuu wa chuo hicho, Prof. Ndelilio Urio. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Mbarawa atangaza mfumo mpya ujenzi wa barabara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa ametangaza serikali inaanza kutumia mfumo mpya wa kisasa wa 'EPC Plus Finance' ambao katika nchi nyingine duniani umekuwa ukirahisisha ujenzi wa barabara za kiwango cha lami kujengwa kwa muda mfupi.

Kwa mujibu wa Prof. Mbarawa, mfumo huo utaanza kutekelezwa nchini kupitia miradi mitatu ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara za Mkoa wa Manyara zenye urefu wa kilometa 1,320.

Alisema jana mjini hapa kuwa kwa sasa mkoa huo tayari umeshaunganishwa na baadhi ya mikoa na utaendelea kuunganishwa na mikoa mingine ikiwamo ya Tanga na Dodoma kwa kujengewa barabara za lami. "Kwa mfumo huu wa EPC Plus Finance, maana yake ni kwamba tutakuwa tunakubaliana kwanza na mkandarasi kutekeleza mradi. Akishakubali anaanza kujenga barabara tunamlipa. "Kupitia utaratibu huo, tutajenga mradi wa Arusha/Kibaya (Manyara) hadi Kongwa (Dodoma) wenye urefu wa kilometa 453," alisema.

Alibainisha kuwa kupitioa mfumo huo, barabara hiyo itajengwa kwa muda wa miaka miwili na nusu. Aliutaja mradi mwingine utakaotekelezwa kwa kutumia mfumo huo ni wa Handeni/Kibirashi (Tanga) wenye urefu wa kilometa 460.

Alisema moja ya madhara ya kuendelea kutumia mfumo wa zamani, serikali ingetekeleza miradi hiyo ya ujenzi wa barabara kwa miaka 10.

Katika taarifa yake, Waziri Mbarawa, alisema tayari serikali imeanza kutekeleza mradi wa Mbulu/Hydom ambao kwa awamu ya kwanza unajengwa kilometa 25 kutoka Mbulu hadi Kijiji cha Garbabi.

Alisema mradi huo unajengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 35.1 na Kampuni ya Kimataifa ya Jiangxi Geo Engineering Group Corporation ya China.

# Mchakato kufumua Sera ya Elimu waiva

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Taknolojia imesema mchakato wa kuifumua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Mwaka 2014 pamoja na Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 ili kuendana na mabadiliko ya elimu duniani, umeiva.

Jana Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Omary Kipanga alisema jijini hapa kuwa serikali imefikia uamuzi huo kwa kuwa duniani kote kumekuwa na ukuaji wa teknolojia, ambao umeleta ongezeko kubwa la taarifa na habari kutoka vyanzo mbalimbali vya habari.

Kipanga aliyasema hayo alipofungua kongamano la pili la kitaifa la huduma za maktaba, tamasha la vitabu na usomaji wa vitabu lililofanya jijini hapa.

"Mkae mkao wa kula, ile sera ya elimu tunakwenda kuifanyia marekebisho tena, lakini si hayo tu, pia sheria zetu za elimu tunakwenda kufanya hivyo hivyo ili kukidhi mahitaji ya sasa ya ubora wa elimu unaohitajika duniani.

"Kongamano hili limekuja wakati mwafaka kwa sababu kama taifa tunataka kukabiliana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoendelea duniani.

"Katika mabadiliko hayo, sera hizo ni lazima ziakisi mahitaji ya kijamii. Hivyo, mitaala inayoongoza kwa ajili ya mafunzo, iongoze pia upatikanaji wa walimu, wakufunzi na wahadhiri na iende sambamba na upatikanaji wa wakutubi mahiri," alifafanua.

Alisema Sera ya Taifa ya Taarifa na Huduma ya Maktaba nayo ni miongoni mwa huduma zinazohitaji maboresho makubwa ili kukidhi mahitaji ya sasa ya jamii.

Awali Mkurugenzi wa Bodi ya Maktaba nchini, Dk. Mboni Ruzegeya, akizungumza katika kongamano hilo, alitaja matatizo kadhaa yanayoikabili bodi hiyo ikiwa ni pamoja na uhapa wa wakutubi na ukosefu wa majengo.

"Kuna baadhi ya maeneo shughuli za maktaba zinafanyika katika majengo ya halmashauri, jambo ambalo linatuwia ugumu kufanya shughuli kwa muda unaotakiwa kutokana na majengo hayo kufungwa muda ambao sisi tunaendelea na kazi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, akijibu hoja hizo, alisema amepokea ombi la kutenga maeneo, lakini suala hilo litawasilishwa wizarani na kusubiria kutolewa mwongozo wa waziri mwenye dhamana.

"Tunamwombea Waziri wa Elimu ni vizuri akatuletea mwongozo haraka kutuelekeza ni wapi tunatakiwa tutenge maeneo, sisi tutatekeleza, na hii imekuja ni ombi kutoka kwa bodi, tukiletewa mwongozo mimi nitatoa maelekezo kwenye halmashauri," alisema.



## Mtafiti ashauri kufanyika mapitio sheria za madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MTAFITI wa Madini, Dk. Dalaly Kafumu amesema kuna haja serikali ikafanye mapitio upya ya sheria za madini zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2017 ili kuondoa vipengele vinavyoogopesha wawekezaji wa sekta hiyo.

Akizungumza jana kwenye Jukwaa la Uziduaji lililoshirikisha wadau wa madini, wakiwamo wachimbaji likiandaliwa na Taasisi ya HakiRasilimali jijini hapa, Kafumu alisema hali si mbaya kwa sasa lakini kama zikirekebishwa itakuwa vizuri zaidi.

Dk. Kafumu ambaye aliwahi kuwa Kamishna wa Madini nchini na Mbunge wa Igunga (CCM) alisema: "Tulikuwa tunaishauri serikali iziangalie tena hizi sheria hususan mambo ya kodi. Kuna sheria ambazo zinaonyesha watafutaji wa madini kutozwa kodi na ni vizuri kuhakikisha anayetozwa kodi ni anayezalisha madini ili kuhamasisha utafiti."

Alisema utafiti wa kugundua madini ulivyoanza mwaka 1998, uliendelea hadi mwaka 2015 lakini haukuendelea mwaka 2017 kutokana na marekebisho ya sheria hizo yaliwaogopesha wawekezaji.

"Ni muhimu sana kuhakikisha wagunduzi wanakuja tena nchini ili kugundua na kuyachimba tena," alisema Kafumu na kuongeza kuwa sheria hizo zinataka kila mkataba utakaoingiwa na serikali na kampuni ya madini, lazima upite bungeni kabla ya kupitishwa, jambo hilo ambalo limekuwa halifanyiki.

Mkurugenzi Mtendaji wa HakiRasilimali, Adam Anthony alisema kuna kero nyingi katika sekta ya uziduaji ikiwamo ushiriki wa makundi maalum, hasa wanawake na faida inayopatikana katika jamii ambazo zinazunguka migodi.

Alisema HakiRasilimali imekuwa ikifanya utafiti kwa kuwashirikisha wadau wengine ili kuzungumza na kubadilishana uzoefu, jambo ambalo wamekuwa wakilifanya kwa muda mrefu.

Mwakilishi kutoka kampuni ya Madini ya Kabanga, Gerald Mturi alisema katika jukwaa hilo wanaangalia jinsi Tanzania itakavyotoka katika matumizi ya nishati zinazozalisha hewa ukaa.

# Serikali yabaini tatizo upatikanaji wa nyama

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema mifugo mingi iliyopo nchini ni ya asili, hivyo uzalishaji wa nyama na maziwa ni mdogo.

Ndaki aliyasema hayo jana wilayani hapa alipogawa madume bora 50 ya ng'ombe aina ya boran, kila moja likiwa na uwezo wa kupanda majike 25 kwa mwaka, kwa vikundi vya wafugaji ili kuboresha mifugo yao ambayo mingi ni ya asili.

Alisema kutokana na hali hiyo, wameanza kuboresha mifugo kwa kutumia madume hayo pamoja na njia ya uhimilishaji ili kusaidia wafugaji kuwa na mifugo michache ambayo itakuwa na uzalishaji mkubwa wa nyama na maziwa.

"Ng'ombe wa asili huzalisha nyama kilo 80 hadi 120 wakati baada ya kuboreshwa kwa kosaafu, mfugaji anaweza kupata kilo 150 hadi 200 kwa ng'ombe, na maziwa ng'ombe hawa walioboreshwa kosaafu huwa na uwezo wa kutoa kati ya lita tano na 10 za maziwa na hivyo kumfanya mfugaji apate tija zaidi tofauti na mfugaji wa asili," alisema.


Waziri huyo alisema ugawaji wa madume bora ya ng'ombe ni utekelezaji wa mpango wa mabadiliko wa sekta ya mifugo na kuwataka wafugaji kuyatunza madume hayo kwa kufuata taratibu zote walizoelekezwa na wataalamu wa mifugo.

"Ninavitaka vikundi ambavyo vimepatiwa madume hayo kuyatumia kwa kushirikiana na wafugaji wengine ili kuhakikisha tija inapatikana kwa wafugaji ndani ya Wilaya ya Chamwino," aliagiza. Kaimu Katibu Mkuu Sekta ya Mifugo, Dk. Asimwe Rwiguza alisema wizara inaendelea kutekeleza mpango wa mabadiliko wa sekta hiyo, akibainisha kuwa mbali na uboreshaji wa kosaafu unaoendelea, pia wanatoa elimu kwa wafugaji kuhusu malisho ya mifugo.

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya aliahidi kusimamia utekelezaji wa mpango wa mabadiliko wa sekta ya mifugo kwa kuhakikisha madume hayo yaliyogawiwa kwenye vikundi, yanatunzwa na kutumika ili kuboresha kosaafu.

Awali Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Maendeleo ya Masoko kutoka Sekta ya Mifugo, Stephen Michael alisema takribani asilimia 97 ya ng'ombe waliopo nchini ni wa asili, hivyo katika kutekeleza mpango wa mabadiliko wa sekta, wizara imepanga kununua mitamba 1,160,000 ambayo itapelekwa kwenye mashamba ya serikali.

"Wizara inaendelea na uhimilishaji mifugo ambapo tayari imeshapanga kuhimilisha takribani ng'ombe 373,000 katika mwaka wa fedha 2022/23 kwenye maeneo ambayo hawatapata madume hayo," alisema.




Waziri mstaafu, Mhandisi Christopher Chiza (kushoto), akipokea kitabu cha mwongozo wa mwanachama kutoka kwa Meneja kutoka Kurugenzi ya Fedha ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma (PSSSF), Michael Bujiba, alipotembelea banda la PSSSF, katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Kifedha, yanayoendelea jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali kuwatengenezea mafuta watu wenye ualbino

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma inatarajia kuanza kutengeneza mafuta kwa ajili ya watu wenye ualbino ili kuwakinga dhidi ya athari za mionzi ya jua. Mratibu wa Tiba wa hospitali hiyo, Dk. Baraka Mponda alibainisha hayo jana jijini hapa alipotoa msaada wa mafuta yaliyotolewa na serikali kuwasaidia watu hao.

Alisema uzalishaji wa mafuta hayo utaanza mwishoni mwa mwaka huu.

"Tunatarajia kuanza kutengeneza mafuta haya ili kuhakikisha yanapatikana muda wote na kwa unafuu kwa ajili ya watu hao wenye ualbino," alisema.

Alifafanua kuwa mkoa huo kijiografia na hali ya hewa, muda mwingi unakuwa na jua kali, hivyo kupatikana kwa mafuta hayo kutalisaidia kundi hilo.

"Tutakuwa na mwendelezo wa kupata mafuta haya kwa sababu sasa hivi tuna wataalamu wa ngozi, wakishirikiana na wafamasia, wameweza kuona 'formula' namna mafuta haya yanavyotengenezwa. Kwa hiyo, kama Hospitali ya Rufani ya Mkoa tupo katika mchakato wa kutengeneza mafuta hapahapa," alisema Dk. Mponda.

Daktari Bingwa wa ngozi, Dk. Peter Chapa alisema mafuta hayo ni muhimu katijka kuwakinga watu wenye ualbino dhidi ya athari za mionzi ya jua.

Aliwataka walengwa waliopatiwa mafuta kutumia kwa uangalifu mkubwa na kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mmoja wa wanufaika hao, Munde Elias aliishukuru serikali kwa kuwapatia mafuta hayo ambayo awali iliwalazimu kuyapata kwa gharama kubwa.

Elias ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), alisema kutengenezewa kwa mafuta hayo kwenye hospitali hiyo kutawapunguzia gharama za kuyapata.





## Wajipanga kupanda mikoko dhidi ya mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKAZI wa kijiji cha Kizimkazi mkoa wa Kusini Unguja wamejipanga kudhibiti mazingira yanayochangiwa na mabadiliko ya tabianchi kwa kuotesha miti aina ya mikoko ambayo ni maarufu katika kulinda mazingira na mmomonyoko wa ardhi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kulinda Hifadhi ya Mazingira ya Unguja Ukuu, Iddi Hassan Ali, alisema hayo jana alipozungumza na waanadishi wa habari wanaofuatilia habari za mazingira.

Alisema wameamua kuotesha Mikoko katika eneo lenye ukubwa wa ekari sita baada ya kubainika athari za mazingira kwa wananchi kukata miti hiyo kwa zaidi ya miaka kumi.

Alisema tayari miti aina ya mikoko milioni 2.8 imeoteshwa katika eneo hilo hatua ambayo itasaidia kurudisha uhai wa eneo ambalo limeanza kushambuliwa na kasi ya maji ya bahari kuja maeneo ya nchi kavu.

"Tumefanikiwa kulirudisha eneo sehemu kubwa ambalo limeathirika na kasi ya uharibifu wa mazingira kwa watu kukata miti katika eneo hili na kutishia uharibifu mkubwa wa mazingira"alisema.

Katibu wa Kikundi cha ZAVECO, Abdi Mgeni Juma, alisema wananchi 150 wamejiunga na jumuiya hiyo kwa ajili ya kulinda mazingira katika eneo la ukanda wa Unguja Ukuu huku wakijikita zaidi na kuotesha mikoko.

Alisema walianzisha kikundi hicho baada ya kujitokeza kwa athari kubwa za ukataji wa mikoko katika eneo hilo kwa matumizi ya kuni, mkaa na kazi za ujenzi wa nyumba. Sheha wa Unguja Ukuu, Khamis Ibrahim Shomari, alipongeza juhudi za wananchi wa kijiji hicho kwa kuunda jumuiya hiyo iliungwa mkono na wananchi pamoja na raia wa nje katika kulinda mazingira.

Alisema kijiji cha Unguja Ukuu pamoja na maeneo jirani ya kisiwa cha Uzi ni maarufu kwa uzalishaji wa mikoko ambayo kwa asilimia 90 eneo hilo limezungukwa na miti hiyo katika ukanda wa fukwe.

Alisema ukataji mikoko umesababisha athari kubwa ikiwamo maji ya bahari kuja juu na kukaribia maeneo ya makazi ya wananchi kutokana na kukatwa kwa mikoko ambayo huzuwia mawimbi ya bahari.

# Waziri aagiza ukaguzi vyombo usafiri majini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk Khalid Salum Mohammed, amesema kipindi cha mwisho wa mwaka idadi ya abiria hasa wanaotumia vyombo vya usafiri baharini kama meli na boti huongezeka, hivyo ni vyema kwa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA) kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vyombo hivyo.

Aliyasema hayo jana katika ofisi za ZMA, Malindi mjini Zanzibar, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuimarisha usimamizi wa usafiri wa abiria kwa njia ya bahari.

Dk. Khalid alisema Novemba na Desemba, mwaka jana, abiria waliosafiri kupitia bandari ya Malindi kwa mwezi ni wastani wa abiria 131,079 wakati katika miezi ya Februari hadi Oktoba, waliosafiri kila mwezi walikuwa wastani wa abiria 106,083.

Alisema ongezeko hilo la abiria hutokana, pamoja na sababu zingine, kufungwa kwa shule, mapumziko ya Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya na ujio wa watalii wengi.

Kwa mujibu wa Waziri, ongezeko la abiria husababisha kuongezeka kwa mahitaji ya usafiri, hivyo serikali itahakikisha wananchi wanapata huduma ya usafiri wa uhakika na salama.

"Pia serikali itahakikisha kuwa meli pamoja na boti zote zinazosafirisha abiria katika nchi zimetimiza viwango vya kiusalama na hazipakii abiria zaidi ya kiwango kilichoruhusiwa kisheria," alisema.

Dk. Khalid alisema katika kipindi kama hiki, hujitokeza watu wachache wanaojihusisha na uuzaji wa tiketi bila vitambulisho na kwa bei ya ulanguzi jambo ambalo husababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi. Aliagiza vyombo husika kudhibiti suala hilo. Aidha, alisema katika kipindi kama hiki pia baadhi ya wamiliki wa meli huuza tiketi zaidi ya kiwango cha abiria walioruhusiwa kisheria jambo ambalo husababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi na wasafiri wengine wanaotumia bandari.

"Kipindi kama hiki pia huko nyuma walikuwapo watendaji wachache wa serikali ambao kwa kushirikiana na baadhi ya watendaji wa kampuni za meli, hawakuwa waaminifu na waliwaruhusu watu wasio na tiketi kuingia bandarini na hatimaye kusafiri bila kuwa na tiketi jambo ambalo ni kinyume cha sheria," alisema.

Waziri huyo alisema serikali imeahidi kuimarisha usafiri baharini ili wananchi kusafiri kwa shughuli zao za kiuchumi na kijamii katika mazingira bora na salama zaidi.

Hata hivyo, Dk. Khalid aliwataka wananchi wapunguze kuchukua idadi kubwa ya watoto wanaposafiri ili kuondoa msongomano na kuhatarisha usalama wao.

Pia aliagiza mamlaka kuziandikia barua kampuni zote zenye meli za abiria kuuza tiketi kulingana na idadi ya abiria ya meli iliyoruhusiwa.



Wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa shahada ya uhandisi wa ujenzi katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume Zanzibar (KIST), wakijifunza kwa vitendo kuhusu maandalizi ya ujenzi wa nyumba, katika taasisi hiyo, Mbweni Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi apigia chapuo wataalamu figo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuna umuhimu kwa taifa kuongeza wataalamu wenye uwezo wa hali ya juu, ili kuongeza ufanisi katika kukabiliana na magonjwa ya figo nchini. Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika Kongamano la Nane la Chama cha Wataalamu wa Magonjwa ya Figo (NESOT), lililofanyika katika Hoteli ya Verde, Mtoni Zanzibar.

Alisema kuna haja ya kuongeza wataalamu wenye uwezo katika kukabiliana na ongezeko la maradhi hayo. Takwimu zinabainisha magonjwa ya figo ni tatizo kubwa linaloikabili Tanzania na dunia kwa ujumla.

Rais Mwinyi aliitaka NESOT wanachama wake kuwa mfano bora wa kuwavutia vijana wapya ili wahamasike kusomea na kujiunga na fani hiyo muhimu, pamoja na chama hicho kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma katika hospitali za rufani na vituo vyote vya huduma za msingi nchini.

Alisema tatizo la figo ni kubwa duniani na takwimu zinaonyesha Tanzania watu saba hadi kumi kati ya watu 100 wanaugua ugonjwa huo.

Dk. Mwinyi alisema katika kukabiliana na hali hiyo serikali imeendelea kuchukua hatua kwa kuongeza vituo vya kutoa huduma za kusafisha damu (hemodialysis) kwa wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo bila malipo yoyote.

"Taarifa njema zaidi ni kwamba tayari mwaka huu matunda yameanza kupatikana baada ya wataalamu 10 kuhitimu masomo yao katika tiba ya magonjwa ya figo," alisema. Pia alisema pamoja na changamoto kadhaa zilizoko katika kuukabili ugonjwa huo, Tanzania imepiga hatua kwa kuanzisha huduma za upandikizaji figo. Zaidi ya wagonjwa 80 tayari wamepata huduma hiyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Dk. Mwinyi aliwataka wataalamu hao kuielimisha jamii kutambua namna ya kujikinga na ugonjwa huo huku na kuzingatia upatikanaji wa lishe bora, kupunguza matumizi ya chumvi na mafuta, kuepuka uvutaji wa sigara, unywaji wa pombe na kudumu katika kufanya mazoezi.

Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema serikali kupitia Wizara hiyo imeweka kipaumbele katika kusomesha wataalamu wa kada muhimu zenye upungufu mkubwa wa wataalamu, wakiwemo madaktari na wauguzi.

Alisema katika kuondokana na changamoto iliyokuwa ikiwakabili wagonjwa wa figo walioko Kisiwani Pemba ya kufuata huduma hizo Unguja, wizara imeweka mashine tano za kusafishia damu katika Hospitali ya Abdalla Mzee, kisiwani humo. Mazrui alisema Wizara inalenga kuweka mashine za kusafishia damu zisizopungua 10 katika kila hospitali ya wilaya, pale ujenzi wake utakapokamilika na kwamba hospitali ya mkoa ambayo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika ifikapo Februari, mwakani, imepangiwa kuwekewa mashine 12 za aina hiyo.




## ASLAY

UKURASA 16

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI NOVEMBA 26, 2022



# DIAMOND ANAJISHANGAA

UKURASA WA 15

YUKO WAPI ?

# FREDDIE KASHEBA-2

## Mchawi wa gita 'kombora', akalivunja na kuzikwa nalo





**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tulianza makala ya mmoja wa wanamuziki mahiri na maarufu sana nchini Tanzania, Freddie Ndala Kasheba.

Huyu ni mtunzi, mpangaji wa muziki, kiongozi na mpiga gitaa la solo aliyekuja na staili ya pekee ya kupiga gitaa la nyuzi 12 nchini Tanzania aliyezaliwa Lubumbashi mwaka 1946.

Wiki iliyopita tuliishia jinsi wanamuziki wenzake wa Orchestra Fauvette walivyotoka Congo DR na harakati zao za kuingia nchini kwa kutumia mashua za walanguzi wa chumvi na kisha kuvuka Ziwa Tanganyika hadi Tanzania kwa kupitia Kigoma. Sasa endelea.

Bendi hiyo ilikita makazi yake kwenye ukumbi wa White House, Ubungo wakati huo ilikuwa mbali na mji, hivyo kulikuwa na ajali nyingi za barabarani ziliwapata mashabiki wa bendi hiyo wakati wa kwenda au kutoka kwenye muziki, hivyo kwa ushauri bendi hiyo ilihama na kuweka kambi kwenye ukumbi wa Mikumi Tours uliokuwa maeneo ya Tazara, Buguruni, wakiporomosha muziki wake siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili.

Ilikuwa ni balaa tupu kwani wakazi wa Dar es Salaam walikuwa hawashikiki. Ni bendi iliyoleta mapinduzi makubwa ya muziki wa dansi nchini, ikichukuliwa kama ni bendi ya kwanza kutinga nchini na kuwa chanzo cha bendi nyingi na wanamuziki kutoka Zaire, ikiwemo Maquiz Du Zaire kuja nchini.

Ilijichukulia umaarufu mkubwa kwa muda mfupi baada ya kurekodi vibao ambavyo viliondokea kupendwa mno hadi leo hii kama 'Camarade ya Nzela' ambao mwenyewe Kasheba alieleza ni wimbo uliokuwa ukizungumzia rafiki wa kukutana nae barabarani au njiani, ambaye roho yake huwa kama sanduku la nguo ndani yake huwezi kujua kuna nini.

Nyimbo zingine maarufu kabisa ni kama 'Nono Na Kalemie', ambao alitungiwa mwanadada mmoja alitwaye Nono mkazi Kalemie chini Zaire wakati huo sasa ikijulikanana kama Congo DR ambaye alikuwa shabiki mkubwa wa bendi lakini walikuwa amemuacha huko kwa ajili ya kutafuta maisha, 'Jacqueline', 'Promesse Azali Nyongo', 'Zula' na 'Francisca'.

Nyimbo zingine zilizowapatia umaarufu ni 'Maria Mwana Kampala', 'Nakanisi Mboka', 'Vivi', Voyage Emonani', 'Bigudi Mwana Teuwen', 'Melinda', 'Mama Nakupenda', 'Maria Sala Tobalana' ambazo zote hizo gitaa la solo alipiga Kasheba na pia asilimia 90 za nyimbo zote alitunga yeye.

**Arejea kwao**

Baadaye ni kama walikumbuka kwao, Fauvette ikiwa na Kasheba ilirejea nchini Zaire (Sasa Congo DR), lakini ndiyo wakati kulikuwa na vuguvugu la kubadilisha majina ya watu, bendi, barabara, mitaa kutoka kwenye majina ya kikoloni na kurejea kwenye majina ya asili.

Katika utaratibu huo rais mwenyewe ambaye jina lake ni Joseph Desire Mobutu akajiita Mobutu Sese Seko Kuku Ngbendu Wa Zabanga.

Wanamuziki wengi walibadilisha majina yao, mfano Franco sasa anachukua jina la Lwambo Luanzo Makiadi, na Rochereau akawa Tabu Ley, bendi ya kina Kasheba nayo Fauvette, ikalazimika kubadilisha jina na kujiita Safari Nkoy, ikiwa na maana 'Chui Msafiri', na ilirejea nchini Tanzania ikiwa na jina lake hilo jipya, ikiwa na wanamuziki wale wale, kina Kasheba, huku kwenye uimbaji wakibaki wale wale, King Kiki na Baziano Bweti.

Walifyatua nyimbo zingine ambazo ni 'Fula Matamba', 'Zinzele', 'Luka Yayo', 'Sina Ndugu' na Mijumbe na Kasongo'.

## UDAKU TU



# Diamond anajishangaa, mashabiki wanamshangaa

KUMEKUWA na minong'ono ya muda mrefu kwa wapenzi wa muziki wa Bongo Fleva, kuhusu mwonekano mpya wa msanii nyota, Diamond Platnumz.

Kila kukicha umbo la Diamond ambalo lilipambwa kwa misuli na tumbo lililoga-wanyika vipande sita, linazidi kupungua kiasi ambacho anaonekana kama mvulana mdogo.

Licha ya kubadilisha mitindo yake ya nywele na mavazi, bado mwili wake haujifichi kuwa hauko katika hali ya kawaida, jambo ambalo linawapa wasiwasi mashabiki wake.

Katika moja ya picha ambazo msanii wake, Mbosso Khan ameposti, Diamond amefika na kuonekana akishangaa kutokana na kuendelea kupunguka kwa mwili wake.

"Halafu nimekuwa mdogo, kila siku nazidi kuwa mdogomdogo. Hilo suala linawachanganya Watanzania wengi," anasema Diamond.

Pamoja na Diamond mwenyewe kujishangaa, kwa nini anazidi kupungua kila siku na kuwa kama mtoto, bado ukweli atabaki kuwa nao mwenyewe nini kinamfanya kuwa hivyo.

Siku za hivi karibuni baadhi ya watu wamekuwa wakimshangaa zaidi kutokana na mwonekano wake huo mpya, na zaidi jinsi anavyojiweka kuanzia mtindo wake wa nywele na hata mavazi.

Wakati wengi wapo katika mshangao huo, wapo wanaojua tatizo linalomsumbua kwa sasa Diamond, hivyo wanatakiwa kuchukua nafasi yao kutafuta ufumbuzi.

Kimsingi watu wa karibu wanaweza kufahamu au kuhisi mwanamuziki huyo ambaye ndiye alama ya sanaa nchini kitu gani kinamsibu, na vipi wanaweza kumnasua.

Kama mwenyewe anakiri kujishangaa, Watanzania nao wanamshangaa, basi wanaojua tatizo wachukue hatua za haraka ili kuepuka mishangao.

Pamoja na wasanii kuwa na tabia za kubadilika kama vinyonga ili kulinda jina na umaarufu wake, bado kwa Diamond inaleta wasiwasi.

Watu wanapenda kumuona na mwonekano nadhifu, unaovutia na wenye kuonyesha utanashati zaidi, ni muhimu kurudi katika mtazamo ule pendwa.

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**@zarithebosslady**
Ninafanya kazi kwa bidii kwa sababu siwezi kuharibu naangalia nyuma, nenda hakuna mtu wa kuangukia na hiyo, hapo ndio motisha yangu.



**@Ishamsaford**
Nikiandika kitabu changu kuhusu mahusiano yangu kuna



**@starshine_tz**
Ukubwa wa Mwenyezi Mungu haupimwi



**@tabumtingita**
Asubutuu wee



**@stevenyerere2**
Mstaafuuu...Siku moja niliwakuta vijana wamekaa wanalalamika wanawake wameisha hamna wanawake, nikaingia na kusema sawa wanawake hamna, je hao wanaume wapo?

BASI SAWA

## Aslay sasa zamu yake



MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Aslay Isihaka amesema sasa ni wakati wake wa kuzungumza baada ya ukimya wa muda mrefu.

Katika ujumbe wake kwenye ukurasa wake wa Instagram, amesema kipindi ambacho aliamua kunyamaza mengi yamezungumzwa, hivyo umebaki wakati wake wa kuongea.

Msanii huyo ambaye ni mwandishi na mtayarishaji wa muziki kwa sasa amesainiwa lebo ya Sony Music Africa.

## Mzee Yusuph akerwa wizi



MWANAMUZIKI mkongwe wa taarabu nchini, Mzee Yusuph, ameonyesha kukerwa na wizi wa kazi za kisanii zinazofanywa na baadhi ya watu.

Amesema wasanii wa taarab wananyonywa kutokana na wizi huo ambao unafanywa na watu waliokuwa ndani ya tasnia hiyo kwa kutoa kopi majukwaa ya mitandaoni.

"Wasanii tunajikuta tunanyonywa jasho letu, unaweza kutoa nyimbo yako na kutumaini unaweza kuuza kupitia mtandao, lakini utakuta tayari kuna mtu kauchukua na kutoa kopi," amesema Mzee Yusuph.



## MAMA DANGOTE AMKUBALI ZUCHU?

MAMA mzazi wa mwanamuziki nyota nchini, Diamond Platnumz, hatimaye amemtaja Zuchu kama mkwe wake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Mama Dangote aliandika ujumbe wa kumtakia Zuchu heri ya kumbukizi kuzaliwa kwake na mwishoni alimtaja jina la Mkwe.

Kuna minong'ono kwamba Zuchu na Diamond licha ya kufanya kazi katika lebo moja ya WCB, pia wanajihusisha kimapenzi japo wote wawili hawako tayari kuweka wazi.



## Muoneeni huruma Mr T Touch

MASHABIKI wamekuja juu baada ya kumsikia mtayarishaji maarufu wa muziki nchini, Mr T Touch, akilalamika juu ya kutishiwa maisha.

Mr T Touch kupitia ukurasa wake wa Instagram alimtuhumu mwanamuziki Chid Benzi anahusika kwa lolote litakalomtokea katika maisha yake baada ya kumuwinda na genge lake la kihuni.

"wamenifuata zaidi ya mara nne au tano kutaka kunifanyia fujo na kunipiga,lakini walishindwa kutokana na mazingira jinsi yalivyokuwa," ilisema sehemu ya ujumbe huo.

FILAMU

## Malkia wa Muhonda: Panda juu ukazibe

**Na Adam Fungamwango**

BINADAMU hawezi kuzuia Mwenyezi Mungu alilolipanga, ila kuna watu wanasema kuwa anaweza kuchelewesha tu.

Ni kama kuichelewesha mahakama, lakini hukumu ipo pale pale.

Hii inatufundisha kuwa binadamu tuache kuhangaika na kuwafanyia wenzetu fitina ili kuzuia wasipate kitu ambacho wanatarajia kupata, kuwanyang'anya au kutaka kuwadhuru.

Hebu tuiangazie filamu ya 'Malkia ya Mhonda'. Ina mafundisho kama haya ambayo nimeyaainisha.

Imechezwa na Juma Kigobora, Angel Hamisi, Mariam Yassin, Fadhili Msisiri na wengineo.

Mzee Mangapi anaishi na mkewe. Wanaishi na mabinti wawili, mmoja Sibo na mwingine Dona.

Sibo ambaye ni mdogo, ni mtoto wa mzee Mangapi ambaye amezaa na mke aliyenaye kwa sasa. Dona ni mkubwa, mzee Mangapi alizaa na mwaname mwingine kabla ya kumuoa huyu. Hilo linaonekana wazi kwenye maisha yao.

Mke wa Mangapi ananyanyasa Dona huku akimpendelea binti yake. Kosa linaweza kufanywa na Sibo, lakini kwa makusudi na mkakati maalum anasingiziwa Dona na anaadhibiwa. Baba naye ametekwa, analazimishwa kupita njia ambayo hatakiwi kupita. Naye bila kujua anajiunga kunyanyasa binti yake.

Dona anakosa raha kiasi cha kumwambia baba yake ampeleke kwa ndugu yoyote wa mama yake kwa sababu amechoma manyanyaso.

Kwenye kijiji hicho mtoto wa mfalme anatahitaji mke. Anaita wanawake wote kwenye hafla ya ngoma. Mke wa Mangapi anamuonya Dona aliende kwenye



hafla hiyo. Anafanya hivyo akitarajiwa kuwa binti yake

"Kesho ni siku ya mtoto wa mfalme. Sihitaji kukuona umefika eneo la tukio, ole wako ukanyage kwa mfalme."Binti akajibu. "Mama sitoenda wala kufika eneo la tukio."

Siku ya tukio, Dona alizuka kwa mfalme, na Kigobora mtoto wa mfalme akamchagua yeye. Mama na binti yake wakakasirika. Wakamroga na kumpa maradhi ya kifafa. Mfalme na mkewe wakamtaka kijana wao achague binti mwingine. Kijana wakakataa katakata. Akawaambia atamuoa hivyo hivyo na ugonjwa wake.

Zamda ambaye ni rafiki wa Sibo na Dona alikwenda kumwambia mwana mfalme kuwa mkewe mtarajiwa hajazaliwa na ugonjwa wa kifafa. Hilo lilimfanya Kigobora kuendelea kufanya uchunguzi. Baba kwa huruma ya binti yake alikwenda kwa mganga na huko ikabainika kuwa mkewe aliyenaye ndiye anayesababisha yote.

Siku ya harusi, mama Sibo akidahani atamroga tena, akajikuta yeye ndiye anaanguka chini. Ni kwa sababu baba alipewa dawa na mganga, ambazo alikwenda kumpa binti yake. Pamoja na mizengwe yote na manyanyaso, Dona anakuwa mke wa mtoto wa mfalme wa himata ya Muhonda. Kijana anaachiwa kiti na baba yake. Dona anakuwa Malkia wa Muhonda.

## BENDI 5 KUTOKA MAJESHI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wa utawala wa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kila shirika na kampuni nchini lilikuwa ama lina timu na mpira wa miguu, netiboli, mpira wa kikapu, ngumi, bendi za muziki wa dansi, taarabu au vyote kwa pamoja.

Na bendi za muziki wa dansi hazikuwa kwenye mashirika na makampuni peke yake, bali hata kwenye majeshi yetu ya ulinzi na usalama.

Leo tutaziangazia bendi za majeshi ya Tanzania. Lengo lilikuwa ni kuwaburudisha makamanda wapiganaji kila wikiendi, wakati mwingine na familia zao.

Kama vile haitoshi, ilikuwa ni kuwapa burudani Watanzania wote, kwani bendi hizo mbali na kupiga makambini, lakini zilikuwa zikipiga kwenye kumbi mbalimbali nchini na zilikuwa zikisafiri nchi nzima.

Kuna wakati bendi za majeshi zilisafiri na kwenda kuburudisha wapiganaji kwenye vita ya Kagera mwaka 1978 hadi 1979.

Kiufupi hazikuwa bendi za mchezo mchezo, kwani zilikuwa maarufu na tishio kwa bendi za raia. Ingawa nyingi bado zipo, lakini si shindani tena kama zamani.

**Mwenge Jazz Band**

Hii ndiyo unaweza kusema kama bendi mama ya zote zilizomilikuwa na majeshi. Wenyewe walipenda kuiita 'Mwenge ya Mashujaa'. Ilikuwa ni bendi tishio na maarufu zaidi ya bendi zote, ikikusanya wanamuziki mahiri nchini Tanzania. Ilikusanya vijana wa Kitanzania wenye vipaji na kuwapa ajira za muziki, na jeshi pia.

Hata hivyo kuna wengine walibakiwa kuwa wanamuziki tu. Bendi hii ipo mpaka sasa, ingawa haina nguvu zile kama za mwanzo ilipokuwa ikishindana na bendi kubwa kama za Msondo na Sikinde.

Inamilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Ilivuma sana katikati ya miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1980.

Nyimbo ambazo zilitia fora na kuifanya bendi hiyo kuheshimika ndani na nje ya nchini ni 'Rehemu', 'Kupatwa kwa Mwezi', 'Mwanahawa', 'Tofali la Barafu','Chenga bin Utoe', na nyingine nyingi.

**Polisi Jazz Band**

Ilikuwa ni bendi ya pili kwa ukubwa na umaarufu kwa bendi za majeshi, ukiondoa Mwenge Jazz Band.

Hii inamilikiwa na Jeshi la Polisi la Tanzania, Makao Makuu yake yakiwa maeneo ya Kilwa Road, maeneo ya Kurasini jijini Dar es Salaam.

Iliwika sana miaka ya 1978, hadi 1981 wakati ilipokuwa na wanamuziki mahiri kama Tx Moshi William, Kassim Mapili, Jalala Ally na wengineo. Ilipendwa mno na mashabiki wa muziki wa dansi Tanzania kwa vibao vyao kama 'Tuli', 'Mwaka wa Watoto', 'Mayasa', 'Wivu Sina' na na nyingine nyingi. Bado ipo, ingawa imepungua makali yake.

**Magereza Jazz Band**

Ni bendi inayomilikuwa na Jeshi la Magereza. Haikuwa maarufu sana kuliko zingine. Lakini kuna wakati ilikuwa ikitoa nyimbo chache zilizopendwa.

Hata hivyo, bendi hii ilijinyakulia umaarufu wa muda mfupi, ilipowachukua wanamuziki kama Abel Bathazar, Hassan Kunyata, Nana Njige na wengineo mwanzoni mwa miaka mwanzoni mwa 1990 na mtindo wao wa 'Mkote Ngoma, Kubali Yaishe' na kutoa vibao vilivyoondokea kuwa gumzo kama 'Edina', 'Ashura' na nyingine nyingi.

**JKT Kimbunga Stereo**

Bendi hii ilikuwa ya kawaida, lakini ilipomchukua John Simon kutoka Nuta Jazz, ndipo ilipoanza kupiga muziki wa ushindani.

Iliwaleta baadhi ya wanamuziki kama Mwarami Said ambaye baadaye alikwenda Sikinde, na kutoa vibao kama 'Cheza Rhumba Kimbunga', 'Ushirikina', 'Chakula Cha Shida' na nyinginezo.

Bendi hii ilimilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

**JKT Mafinga 'Kimulimuli'**

Pia bendi hii ilimilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), lakini haikuwa Dar es Salaam, bali mkoani Iringa. Ilikuwa ni kama kikosi cha pili cha JKT Kimbunga. Ni kwamba baadhi ya wanamuziki walioonekana wamekosa nafasi Kimbunga, walipelekwa Iringa. Walimpata pia Zahir Ally Zorro wakafanya kazi ya maana. Wimbo wao wa kwanza ambao uliwafanya kuanza kuwa maarufu na bendi tishio si kwa JKT Kibunga yenyewe tu, bali hata bendi nyingine ni 'Christina' uliotoka mwaka 1977, uliotungwa na kuimbwa na Zahir.

BONGO FLEVA

# Lilian atamani kuwa kama ...



MWIMBAJI anayechipukia katika nyimbo za Injili, Lilian Naman, amesema anavutiwa na waimbaji mbalimbali wanaotamba kwa nyimbo hizo, akiwamo Christina Shusho.

Lilian amesema hayo mwishoni mwa wiki mara baada ya kuzindua albamu zake mbili za 'Nishike Mkono na Upo Uwezekano' katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Usharika wa Kinyerezi Dar es Salaam.

"Albamu yangu ya kwanza 'Tumaini Limerudi' ambayo ilitoka 2016 nikiwa nimemshirikisha Shusho, kwani ni miongoni mwa waimbaji ninaovutiwa nao kwa uimbaji wa Injili, ninatamani kuwa kama yeye," amesema.

Lilian amesema kazi ya kuimba nyimbo za kumsifu Mungu zinahitaji kujitoa zaidi tofauti na fani zingine za sanaa.

Ameeleza Shusho ni miongoni mwa waimbaji ambao wanajitoa na muugwana kwenye kazi, jambo ambalo linamtia moyo na kuamini siku moja anaweza kumfikia.

"Nyimbo za Shusho zimekuwa zikipigwa katika shughuli mbalimbali, hata mimi ninatamani nyimbo zangu zitumike hivyo, kama mtu ana shughuli yake anaweza akaja tukazungumza nikaenda kutoa huduma," ameongeza kusema.



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Twanga Pepeta**

Kila Ijumaa huwa wanatoa burudani ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, Pweza Beach Kigamboni na kesho Jumapili watamalizia wikiendi katika ukumbi wa Gwambina Lounge, zamani TCC Club Chang'ombe.

**Town Classic Band**

Jana wakiwa na wenzao wa bendi ya Waluguru Original, walifanya vitu vyao katika uwanja wa Jamhuri mjini Mogorogo, leo wataendelea kuwa pamoja katika ukumbi wa Termin Pub, kesho ndani ya F2 Florida.

**Orchestra Sikinde Original**

Bendi hii mpya leo Jumamosi inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Beach, kesho Jumapili kama kawaida itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**FM Academia 'Wana Ngwasuma'**

Leo Jumamosi kama kawaida yao wakiwa chini ya Patcho Mwamba, watatoa burudani katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo, uliopo kando ya barabara ya Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam.

**Tukuyu Sound Band**

Kama kawaida yao, kila Jumapili vijana wa bendi hii watamalizia wikiendi yao katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park, uliopo Ubungo kando ya Barabara ya Sam Nujoma.

Orchestra Sikinde Original

Bendi hii mpya leo Jumamosi inafanya vitu vyake katika ukumbi wa Shabaha Mbezi Beach, kesho Jumapili kama kawaida itakuwa katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**Kimokimo Band**

Wakiwa chini ya mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa huwa ndani ya ukumbi wa Mariot uliopo eneo Extertanal jijini Dar es Salaam.

**Mjengoni Classic Band**

Bendi hii ya jijini Arusha, leo Jumamosi itafanya makamuzi yake katika ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**Waluguru Original**

Baada ya onyesho la jana, leo wakishirikiana na bendi ya Town Classic katika ukumbi wa Terminal Pub Msamvu na Jumapili wote watakuwa ndani ya ukumbi wa ukumbi wa F2 Florida mjini Morogoro

**Maina Band**

Bendi hii inayoongozwa na mwimbaji mkongwe, Liston Maina, leo Jumamosi itafanya makamuzi ya nguvu katika ukumbi wa Regancy Park, Mikocheni.



# NDOTO ZA KANYE WEST

RAPA maarufu kutoka Marekani, Kanye West kila kukicha anawashangaza watu kutokana na kauli zake tata, hivi safari hii amekuja na mpya na kutaka mashabiki wake kumuunga mkono.

Kanye kupitia ukurasa wake wa Instagram, ametangaza nia yake ya kugombea nafasi ya urais wa Marekani mwaka 2024, lakini amemuomba Rais wa zamani Donald Trump, kuwa mshirika wake.

Katika uchaguzi wa mwaka 2020, West alikuwa akimuunga mkono Donald Trump katika kinyang'anyiro cha urais.

Rapa huyo ambaye hivi karibuni amepoteza mamilioni ya pesa kutokana na kauli yake moja, ametangaza nia yake ya kugombea uchaguzi wa rais wa Marekani uliopangwa kufanyika mwaka 2024.

Katika video ya hivi majuzi akihojiwa na wanahabari walimuuliza mwimbaji huyo iwapo atawania tena urais.

"Kwa hili, nijibu kwa kuthibitisha kwamba ni rahisi. Tunasonga mbele," alijibu.

Akiashiria mwanasiasa Milo Yiannopoulos, ambaye pia alikuwa kwenye video ya rapper huyo na mfanyabiashara tajiri alisema, "Huyu ni Milo anafanya kazi kwenye kampeni."

Tangu kufichua kwa nia yake hiyo, West amekuwa akiwaweka watu kwenye njia panda kuhusu malengo yake atakapoingia katika kinyang'anyiro hicho.

Kana kwamba haitoshi, mwanamuziki huyo alifichua kwamba alikutana na rais wa zamani Donald Trump kujadili uchaguzi ujao.

Akitumia ukurasa wake wa Twitter, aliandika "Mara ya kwanza huko Mar-a-Lago. Mvua na trafiki hawawezi kuamini kuwa nilimsubiri Rais Trump. Na nilikuwa nimevaa jeans na nilichapisha kura kwa mashabiki wake,"

"Mnadhani jibu lake lilikuwa nini nilipomwomba awe mgombea mwenza wangu mnamo 2024?" amehoji West.

Hii ni mara yake ya pili kutaka kuwania nafasi ya urais. Mwaka 2020, West alijaribu kuweka nia yake ambayo haikufanikiwa. Alikubali kutoendelea katika kampeni baada ya kujitokeza kwenye kura katika majimbo 12 tu kati ya 50 kutokana na kupata kura chache.

Kabla ya azma yake ya kuwania urais, rapper huyo alimuunga mkono hadharani Trump na alimtembelea Ikulu ya White House akiwa amevalia kofia yake maarufu ya "Make America Great Again" na kusababisha Wamarekani weusi kumchukia.

Trump, ametangaza kugombea Urais mwaka wa 2024 baada ya kuhudumu kwa muhula mmoja kama rais wa 45 wa Marekani kati ya 2017 na 2021.

Wote wawili walirejea Twitter hivi karibuni. Wakati Trump alipigwa marufuku kutoka jukwaani baada ya ghasia za Januari 6 katika Ikulu ya Marekani mwaka jana, West aliondolewa kwa maoni yake ya chuki dhidi ya Wayahudi.



# Canon sasa hiyo sifa

MWIGIZAJI Canon na mkewe Abby De Le Rosa wanathibitisha kwamba wanatarajia kupata mtoto wa 12 na kuifanya famialia kuwa kubwa.

Canon amefichua kuwa kipaumbele chao ni watoto akisema wao ndio nguvu ya ubunifu.

"Namaanisha hicho ndicho kipaumbele changu cha kwanza, ninaamka nikiwa baba nikifikiria watoto wangu na kila kitu kingine kinachokuja baada ya hapo," amesema Canon.



## Julia uliyoyataka umeyapata

Mwigizaji wa Kiitaliano mwenye asili ya Marekani Julia Fox ametoa siri ambayo imemfanya kutoka kimapenzi na Kanye West.

Fox amesema ilikuwa ni njia ya kumtoa kwenye mgongo wa Kim Kardashian ambaye wameachana kwa sasa.

Hivi majuzi kuliibuka na mjadala kuhusu uhusiano wake mfupi na rapa wa Marekani.

## Rita, Fidelis kubariki ndoa Uingireza

MWIGIZAJI nyota wa Nollywood Rita Dominic na mwenzi wake, Fidelis Anosike, watakula kiapo cha ndoa katika sherehe ya harusi nchini Uingereza.

Katika taarifa zilizothibitishwa zinasema ndugu na marafiki watahudhuria katika sherehe hiyo ya kubadilishana kiapo cha wanandoa hao katika kanisa moja la nchini Uingereza yenye umri wa miaka 900.

Awali, wawili hao walifunga ndoa ya kitamaduni Aprili mwaka huu.





## Buju, Ruger wako vitani

BIFU liloibuka kati ya wanamuziki wawili wa Nigeria, Buju BNXN na Ruger, limewaibua mastaa mbalimbali kwa kueleza maoni yao mbalimbali.

Blaqbonez na Yemi Alade waliingia mtandaoni na kumjibu Buju ambaye anadai Ruger anatumia mashabiki feki kuongeza namba katika chati ya muziki ya Aple ambayo ni maarufu nchini humo.

Blaqbonez amesema inaumiza kumuona mwanamuziki analalamika kutokana na mafanikio ya mwenzake, ni wazi kupanda alama katika chati inatokana na ubora wa kazi pekee.

## Kizz Daniel awasha moto Qatar.

Nyota wa muziki wa Nigeria Kizz Daniel, usiku wa kuamkia juzi alipanda jukwaani nchini Qatar na kuwasisimua mashabiki wa soka kwa baadhi ya nyimbo zake kali.

Hii inakuja baada ya msanii huyo kueleza nia yake ya kutaka kutumbuiza kwenye michuano ya Kombe la Dunia 2023 nchini humo baada ya kuachia wimbo wake wa Buga Many.

Mashabiki na wafuatiliaji wa mwimbaji huyo wamejitokeza kwenye mitandao ya kijamii kumshangilia kwa uchezaji wake unaovutia.





# Utafiti unapobaini maajabu ya tangawizi

## •Yafanya kazi tano kifamasia mwilini

Na Mwandishi Wetu

TANGAWIZI ni kiungo muhimu katika chakula na ipo katika familia moja kama manjano na iliki.

Asili ya mmea huo unatoka Asia ya Kusini Mashariki, India na China.

Tangawizi ni sehemu ya lishe ya eneo hilo na inathaminiwa kwa harufu yake nzuri, kiungo cha upishi na dawa.

Ingawa tunafahamu zaidi mapishi tunayopenda kama vile mkate wa tangawizi, kionjo katika chai imekuwa ikitumika kutokana na sifa zake tangu zamani.

Ndani ya tangawizi inapatikana protini,madini ya Potasiamu, wanga na nyuzinyuzi.

**KUPUNGUZA MAFUA**

Chai ya tangawizi ni chaguo bora kama dawa ya kutibu dalili za awali za mafua. Unapokunywa inakufanya utoe jasho na kwa hivyo inaweza kutumika kutibu magonjwa ya homa kama mafua.

Pia mmea huu aina ya mzizi ikipondwa kama unga inakabiliana na athari za 'antiviral'.

**KUTULIZA KICHEFUCHEFU**

Mizizi ya tangawizi hupunguza kizunguzungu, kichefuchefu, kutapika, na jasho la baridi.

Hali hii inaweza kuenea kwa watu wanaofanyiwa upasuaji ingawa utafiti zaidi unahitajika kupata uthibitisho.

Tangawizi imetumika zaidi kutibu kichefuchefu na kutapika kwa akina mama wajawazito.

Hata hivyo, ukiona dalili hizo zinaendelea unatakiwa kuwasiliana na daktari au mkunga kujua kama unatakiwa kupata matibabu zaidi.

**KUPUNGUZA MAUMIVU**

Sifa nyingi za uponyaji za tangawizi zinahusishwa na zile zenye nguvu za kuzuia maumivu makali mwilini.

Matokeo haya yanaonekana kuwa muhimu yanapotumiwa kwenye sehemu mahususi kwenye mwili.

Hata hivyo, tafiti nyingi zinaunga mkono matumizi ya tangawizi kupunguza dalili za matatizo ya 'osteoarthritis' ambayo yanaathiri mifupa.

Pamoja na hayo, sehemu ya mzizi wa mmea huu inayotumiwa zaidi katika aina za dawa mbadala, ina mafuta mengi tete. Watu wanaougua ugonjwa wa mifupa ambao hutumia tangawizi mara kwa mara, wanaona viwango vyao vya maumivu hupungua na afya kuwa bora.

**KUTULIZA USAGAJI CHAKULA**

Tangawizi ina sifa ya muda mrefu ambayo inasaidia uondoaji wa gesi ya ziada katika mfumo wa utumbo, na inajulikana kutuliza njia ya utumbo.

Vyakula vinavyopikwa kwa kuchanganywa na tangawizi humuwezesha mlaji utumbo wake kusaga chakula kwa umakini na katika utaratibu unaotakiwa.

**KUBORESHA AFYA YA MOYO**

Baadhi ya tafiti za wanyama zinaonesha kuwa tangawizi inaweza kusaidia kudhibiti viwango vya mafuta mwilini, kupunguza uharibifu wa ateri, na kupunguza shinikizo la damu.

Kutokana na upunguzaji huo wa mafuta, watafiti wanakubaliana kwamba mmea huo una faida kubwa katika mfumo wa moyo na usambazaji wa damu mwilini.

**JE, NI SALAMA?**

Ingawa inachukuliwa kuwa tangawizi ni salama kwa hali nyingi, ukweli unabaki kuwa ni mmea wenye nguvu inayofanya kazi kifamasia.

Kwa sababu hiyo, haiwezi kupendekezwa kwa baadhi ya watu wenye matatizo ya kiafya.

Watu ambao hawaruhusiwi kutumia tangawizi ni wale wenye historia ya matatizo ya mawe kwenye figo yenye oxalate.

Pia watu mbao mara nyingi wanakabiliwa na kiungulia au aside pia hawapendekezwi kutumia.

Watu wenye shinikizo la chini la damu au wanaokunywa dawa za shinikizo la damu wanatakiwa kutumia kwa kiasi tangawizi katika mlo wao.

Watu hawa wanapaswa kutumia tangawizi kwa kiasi kutokana na uwezekano wa athari zake kwenye shinikizo la damu.

Ikiwa hauna uhakika kama ni salama kutumia tangawizi, wasiliana na daktari kwanza.

**CHANZO: BBC**



# Rais Obiang anapozeekea madarakani

## •Ajilimbikizia utajiri, mtoto wake sharobaro

Na Mwandishi Wetu

GUINEA ya Ikweta ni nchi ndogo iliyoko Afrika Magharibi, imebarikiwa kuwa ni tajiri wa mafuta, lakini wananchi wake wanaishi katika lindi la umasikini.

Mpaka sasa nchi hiyo ina vyama viwili pekee vya siasa, chama tawala kinachoongozwa na Rais Teodoro Obiang Nguema na chama kimoja cha upinzani kilichoruhusiwa katika siasa nchini humo.

Rais Teodoro Nguema mwenye miaka 80, ndiye kiongozi pekee barani Afrika aliyedumu madarakani kwa miaka mingi.

Akiwa kaongoza nchi hiyo kwa miaka 43, bado anatarajiwa kuchaguliwa tena na pengine kuvunja rekodi nyingine.

Wananchi wa Guinea ya Ikweta kesho wataingia katika vituo vya kupiga kura kumchagua rais na wabunge.

Rais Teodoro Obiang Nguema Mbasogo aliyeitawala nchi hiyo tangu Agosti mwaka 1979, anatarajiwa kushinda muhula wa sita katika uchaguzi huo.

Hata hivyo, pamoja na nchi hiyo kuwa katika lindi la utajiri wa mafuta, kiongozi huyo na familia yake inahodhi utajiri wote kiasi ambacho hakuna mwananchi wa kawaida anayenufaika na mauzo ya mafuta nje.

Kutokana na ukandamizaji wa wapinzani, rais huyo anayeamini kuwa nchi hiyo ni miliki yake ameshuhudia majaribio kadhaa ya mapinduzi.

Alichukua madaraka kutoka kwa mjomba wake Francisco Macias Nguema mwaka 1968 ambaye alikuwa rais wa kwanza wa Guinea baada ya uhuru kutoka Uhispania na baadae kujitangaza kuwa rais wa maisha.

Macias aliuawa na Obiang, kwa kupigwa risasi miezi miwili baada ya mapinduzi.

Hata hivyo, wapinzani wa Rais Obiang wanasema kwamba chini ya utawala wake wa mkono wa chuma, Guinea ya Ikweta imekuwa kama Korea Kaskazini ya Afrika.

Uchaguzi kwa wengi wanaona kama kiini macho, kwani utawala huo licha ya kukosolewa na mashirika ya kutetea haki za binadamu, bado unajizatiti kubaki madarakani.

Mnamo mwaka 2016, Rais Obiang alichaguliwa tena kurudi madarakani kwa asilimia 93.7 ya kura. Katika uchaguzi huo chama chake cha Democratic Party of Equatorial Guinea -PDGE kinategemewa tena kurudi madarakani.

Chama hicho kilikuwa kikishikilia viti 99 kati ya 100 vya bunge na katika baraza la Seneti kinadhibiti viti vyote 70.



Teodorin Nguema Obiang ambaye ni mtoto wa rais wa Guinea ya Ikweta

### AMUANDAA MTOTO WAKE

Mtoto wa Rais Teodoro Obiang Nguema Mbasogo, anayesifika kupenda maisha yake ya kifahari anaandaliwa kushika nafasi yake endapo atastaafu au kufariki.

Mbasogo ambaye ndiye makamu wa rais, anatajwa kuwa na majumba ya kifahari huko California nchini Marekani na Ufaransa.

Maisha yake hayo mazuri ni tofauti na wananchi wenzake wengi, ambao wanafaidika kwa kiasi kidogo na mapato yatokanayo na mafuta.

Mtindo wake wa maisha na matumizi yake yanatajwa kuhusishwa na ubadhirifu.

Hivi karibuni Teodoro alikabiliwa na hatia ya makosa ya kiuhalifu nchini Ufaransa, amewekewa vikwazo nchini Uingereza na kuwa na rekodi mbaya ya rushwa nchini Marekani.

Lakini nchini kwake, Teodoro mwenye umri wa miaka 52 anaendelea kusalia kuwa makamu wa rais, akijiandaa kuchukua nafasi hiyo kumrithi baba yake mwenye umri wa miaka 79.

### VITENDO VYA UBADHIRIFU

Teodoro aliishi California mwaka 1991 alipojiunga na chuo kikuu cha Malibu.

Alinunua nyumba ya kifahari yenye thamani ya dola milioni 30 huko Malibu.

Nchini Marekani pia anamiliki gari la Ferrari na vitu vya thamani vya kumbukumbu ya mwanamuziki Michael Jackson.

Haya yalibainika mwaka 2014 alipoamriwa na mahakama nchini Marekani kusalimisha mali hizo baada ya kubainika zimetokana na matumizi yake ya fedha zinazonuka rushwa.

Mwaka 2016, waendesha mashtaka wa Switzerland walikamata magari yake 11 ya kifahari. Baadhi ya magari hayo; Bugatti, Lamborghinis, Ferraris, Bentleys na Rolls Royce ambayo yaliuzwa kwenye mnada kwa kiasi cha dola milioni 27.

Kiasi cha dola milioni 23 kilipelekwa kusaidia miradi ya maendeleo nchini Guinea ya Ikweta.

2017, Ufaransa ilimbana Teodoro, baada ya kukutwa na hatia na mahakama ya ubadhirifu wa fedha na kuamuru kukamatwa kwa mali zake nchini humo.

Licha ya kutokuwepo Mahakamani, alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu, faini ya dola milioni 35, na mali zake za kifahari Ufaransa zilikamatwa. Moja ya mali zake zilizokamatwa Paris ilikuwa na thamani ya zaidi ya dola milioni 120.



Rais Teodoro Obiang

MAKALA

# Wanaume wengi wavyovumilia vipigo kutoka kwa wake zao

## ■Mila na desturi, aibu yachangia

Na Sabato Kasika

UKATILI wa kijinsia, ni kitendo chochote ambacho mtu wa jinsi yeyote anaweza kufanyiwa bila ridhaa yake kwa nia ya kumdhuru kimwili, kisaikolojia, kiafya, kingono au kiuchumi.

Wanawake, wanaume na watoto, wote ni waathirika wa vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia.

Mara nyingi vitendo vya unyanyasai wa aina hii huambatana na vitisho, kulazimisha au kumnyima mtu uhuru, iwe kwa kificho au kwa uwazi.

hata hivyo, inawezekana baadhi ya watu wakawa wanadhani kuwa wanawake na watoto pekee ndio wanaofanyiwa vitendo hivyo, kumbe hata wanaume nao ni miongoni mwa wanaoumizwa.

Dhana hii imejengeka ndani ya jamii wakiamini vitendo vya ukatili wanafanyiwa wanawake na watoto tu, hivyo imesababisha wanaume wasionekane nao ni sehemu ya walengwa.

Kusambaa kwa taarifa zao kuhusu ukatili wanaofanyiwa na wenza wao, marafiki na hata ndugu, imesababisha kuanzishwa madawati ya jinsia na watoto kwenye vituo vya polisi nchini kwa lengo la kudhibiti.

Wakati vitendo hivyo kwa wanawake na watoto vikiongezeka, serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yamegundua hata wanaume nao wananyanyaswa na wake zao.

### KUFA NA TAI SHINGONI

Sababu kubwa ya wanaume waonapatwa na unyanayasaji ni tabia yao ya kukaa kimya kutokana na mila, desturi na aibu.

Mkurugenzi wa wa Taasisi ya Kaya Foundation ya jijini Dar es Salaam, Anna Pili Ngome wakati akizungumza na gazeti hili anasema kuna wanaume wengi wanadhulumiwa lakini ukimya umetawala.

"Ingawa wengi wa wanaoathirika kwa ukatili wa kijinsia ni wanawake na watoto, lakini wanaume nao wamo, wengine wanauawa, lakini mila na desturi na kuona aibu vinachangia kuwafanya wawe kimya wakiumia moyoni," anasema AnnaPili.

Anafafanua kuwa mila na desturi za baadhi ya makabila haziruhusu wanaume kuonyesha kwamba wao ni dhaifu kwa wake zao, na kwamba wanaamua kuwa kimya hata kama wanaumizwa.

"Nimefanya semina na kushiriki makongamano mengi ya mambo ya jinsia, nimegundua mengi kuhusu unyanyasaji unaohusu makundi yote, lakini wanaume wanaofanyiwa wanaamua kufa na tai shingoni," anaongeza kusema.

Mkurugenzi huyo anasema kuwa umefika wakati sasa wanaume kuachana na tabia ya kufa na tai shingoni, badala yake wafunguke, kwa kuwa hiyo ndio njia itakayosaidia kukomesha vitendo hivyo katika jamii.

"Pia jamii iondoe dhana kwamba wanaofanyiwa ukatili ni wanawake na watoto tu, kwani wapo wanaume wanaopokea vipigo kutoka kwa wake zao ila hawasemi, hebu tuwasaidie wafunguke," anasema.



Mkurugenzi wa Kaya Foundation, Annapili Ngome anayezungumzia vipigo vya wanawake kwa wanaume na kuwataka wasiendelee kuwa kimya. **PICHA: SABATO KASIKA .**

### KUTOA TAARIFA

Baada ya kuona wanaume wamekuwa wagumu kutoa taarifa za ukatili wanaofanyiwa na wenza wao, serikali sasa imeahidi kuweka mifumo saidizi ngazi zote hadi kwenye madawati ya jinsia ili wawe huru kutoa taarifa zao.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anasema hatua hiyo ni kuwafanya wawe na uhuru wa kuyatoa yote ya moyoni.

"Ili kuwasaidia tutaweka mifumo saidizi katika ngazi zote kwenye madawati ya jinsia yawe pia na ya wanaume, tutatoa mkeka wa namba ili wanaume wajitokeze wawe huru kusema katika madawati hayo," anasem Dk. Gwajima wakati akizindua siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Anasema, uvumilivu huo wa wanaume, mwisho wake huwa mbaya kwa kufanya matukio makubwa katika jamii.

Anawataka kujitokeza na kutengeneza mitandao yao ili wawe na sauti moja kama ambavyo wanawake wamekuwa wakifanya.

Aidha, anasema asilimia 40 ya wanawake wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 49,wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili au kingono mara moja au zaidi, katika kipindi cha maisha yao.

"Hizo ni takwimu za Utafiti wa Afya ya Uzazi na Viashiria vya Malaria ya mwaka 2015/16 ambayo inaonyesha kuwa asilimia 20 ya wanawake wa umri huo, wameingiliwa kimwili bila ridhaa yao," anasema waziri Gwajima.

### ATHARI KISAIKOLOJIA

Mtaalam wa saikolojia kutoka taasisi ya Thamani Yangu Initietive ya Ubungo Dar es Salaam, Slyvia Sosthenes, anasema mtu kufanyiwa ukatili na kukaa kimya anapata athari ya kisaikolojia.

"Kama ni mtoto anaweza kutoweka kwao na kwenda kusikojulikana, mwanaume au mwanamke aliyefanyiwa ukatili, anaweza kuwa na hasira za muda mrefu na kujikuta akimvizia mwenza wake na kumuumiza,"anasema Slyvia.

Anafafanua kuwa mwanaume anayepigwa na mkewe, hujihisi kuwa ni dhaifu na mwenye kudhalilika, na kwamba hawezi kuchangia hoja yoyote mbele ya wanaume wenzake.

Msaikolojia huyo anasema ili kupunguza ukatili huo, ni vyema wenza wanaofanyiana vitendo hivyo, wakakaa pamoja na kutafuta chanzo cha ugomvi na hatimaye kupata ufumbuzi.

### HALI IKOJE NCHINI

Taarifa ya matukio ya ukatili iliyotolewa na Jeshi la Polisi kwa waandishi wa habari mwaka jana, inaonyesha kuwa kulikuwa na maatukio 908 ya wanandoa kuuana na kujiua kuanzia mwaka 2019 hadi Septemba 30 mwaka huo.

Msemaji wa jeshi hilo, SACP David Misime akaeleza kuwa wanaume 750 wameua wake zao, huku 74 kati yao wakiwa wamejiua wenyewe na pia wanawake 158 wameua waume zao, 39 kati yao wakiwa wamejiua wenyewe.

Katika mchanganuo wake, SACP Misime anasema wanaaume walioua wake zao mwaka 2019 walikuwa ni 328, huku waliojiua baada ya kuua wake zao wakiwa ni 28. Wanawake walioua waume zao wakiwa ni 58, huku 18 kati yao wakiwa wamejiua baada ya kuua waume zao.

Mwaka uliofuata wa 2020, wanaume walioua wake walikuwa ni 226, kati ya hao 30 walijiua baada ya kuua, huku wanawake walioua waume zao wakiwa ni 71, huku 12 kati yao wakijiua baada ya kuua waume zao.

Hadi kufikia Septemba 30 mwaka jana, wanaaume walioua wake zao walikuwa ni 156, ambao waliojiua baada ya kufanya ukatili huo ni 16, na kwamba wanawake walioua waume zao walikuwa 29, huku tisa kati yao wakijiua baada ya kuua.



Mwanamke akimdunda mwanaaume. PICHA: MTANDAO

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kutoka kuomba maji majumba ya watu hadi kununua ya chupa

**Na Adam Fungamwango**



DUNIA inasonga mbele na nchi imekuwa na maendeleo makubwa. Nakuhadithia kitu ambacho utashangaa. Leo unamuona mtu mitaani anatembea barabarani na chupa yake ya maji ya kunywa. Wakati mwingine ameshika tu chupa, au anakunywa. Kwenye vyombo vya usafiri unakuta abiria wana chupa zao za maji, hawana wasiwasi anaweza kutoka na maji yake kwenye chupa kutoka mkoa mmoja mpaka mwingine, au sehemu moja au nyingine. Anapokuwa na kiu anakunywa. Anapojisikia hamu anakunywa pia.

Hata mtu akitoka kazini akiwa anarudi nyumbani anaweza kununua maji yake, akawa anakunywa taratibu huku akiendesha gari lake, badala ya kusubiri kwenda kunywa nyumbani.

Unaanza kukumbuka miaka ya nyuma. Miaka ya 1990 kurudi nyuma hali haikuwa hivi.

Siyo hakukuwa kabisa na maji cha chupa, hata viwanda vya maji havikuwepo. Yoyote mwenye kiu kama anatembea njiani, akiwa peke yake atalazimika kwenda kuomba maji kwenye nyumba yoyote ile kama atapatwa na kiu ambacho atashindwa kuvumilia mpaka kufika nyumbani.

Hata watu wakiwa kikundi, wawe watoto au watu wazima watalazimika kuiteua nyumba moja iliyo jirani ya sehemu ambayo wamepatwa na kiu, watapiga hodi na mwenyeji akitoka wataomba maji ya kunywa.

Wanafunzi nao walikuwa na mabomba, ambapo walikuwa wakinywa kwa kila mmoja kutumia mikono yake kukinga bombani. Kuna wale waliokuwa ambao hawakuwa wastaarabu walikuwa wakiingiza midomo yao kwenye mdomo wa bomba.

Sikumbuki kama zamani kuna mtu ameshawahi kusema kuwa aliwahi kunyimwa maji ya kunywa. Kipindi kile ilionekana ni dhambi kumnyima mtu maji ya kunywa, "yaani maji ya kunywa tu umnyime mtu, hapana?" Walisema hivyo.

Hata watoto wadogo wanapocheza mpira, wanapomaliza, walikuwa wanakwenda kwenye nyumba yoyote ile kuomba maji ya kunywa na wakapewa.

Anachofanya mwenyeji ni kuingia ndani, muda mfupi baadaye anatoka na jagi, pamoja na kikombe cha bati na wote waliokuwepo watakunywa. Na kama hawajatosheka watakwenda kuchukuliwa mengine ndani.

Kama si hivyo basi kulikuwa na migahawa mingi ambayo zamani ilikuwa inaitwa 'mahoteli' ambayo yalikuwa na mabomba ya maji.

Yeyote mwenye kiu anapotembea njiani akikutana na hoteli basi ataingia na kwenda bombani, atachukua kikombe na kunywa.

Migahawa yote ya zamani ilikuwa inauza chakula tu, lakini siyo maji. Kuna mtu alishangaa sana nilipomwambia kuwa zamani hakukuwa na maji ya chupa. Akanitolea macho na kuniuliza, " sasa mlikuwa mnaishi vipi?" Nikamwambia tulikuwa tunaishi kama hivi niliyoandika.

Ni pale tu unapooona kitu ndiyo utaanza kuangalia uwezekano wa kuomba maji kwenye majumba ya watu.

Huko vijijini, kuna maeneo chini ya miti njiani uliwekwa mtungi wa maji ili mtu yoyote mgeni au mwenyeji akipita anywe.

Lakini mara nyingi maji hayo yaliwanufaisha zaidi watu wanaotoka na kwenda mbali. Yaani anatoka kijiji cha mbali na kwenda mbali pia. Atakuta mtungi wa maji, atakunywa, ataendelea na safari yake.

Nikaulizwa "kumbe hakukuwa na hata chupa za ptastiki?" Nikamjibu ni kweli chupa za wakati huo zilikuwa ni za glasi tu. Na zilipatikana kwenye soda, bia, au juisi zilizokuwa zinauzwa kwenye chupa, ambayo zamani tuliyaita 'maji ya orenji', yale ya rangi ya njano, lakini pia kulikuwa na juisi za maji ya zabibu ambayo tuliyata 'maji ya zabibu.'

Kwa wakati ule ilionekana ni jambo la kawaida tu kwa sababu hakukuwa na mtu yoyote ambaye angeweza kujua kama kuna sehemu kwenye dunia hii watu wananunua na kunywa maji kwenye chupa, tena za plastiki. Kwenye nchi zingine hasa zilizoendelea tayari mambo hayo yalishaingia.

Ni kama vile tulivyoishi kwenye zama za bila simu ya mkononi, mtu akiondoka tu hamuwezi kuwasiliana hadi arudi zaidi ya kutumiana barua.

Na ilikuwa huwezi kumtumia mtu pesa, labda kwa kifurushi kwa njia ya posta na mpaka ifike siyo leo.

Niliandika mwanzo kuwa dunia inasonga mbele kila kukicha, na nchi inakuwa na maendeleo kila kunapopambazuka.

Hizi sasa siyo zama za kugonga hodi na kuomba maji. Wakati ule watu walikuwa wajamaa sana, siku hizi mambo yamebadilika. Na watu pia wamebadilika. Hawaaminiani. Muomba maji na muombwaji kila mtu anamhofia mwenzake.

Kama kusingekuwa na viwanda ambavyo vimetuletea maji ya chupa sijui ingekuwaje. Muombaji anahofu kwenda kuomba kwa sababu ana wasiwasi kama maji yao ni safi na salama au yatakuwaje. Muombwaji naye ana wasiwasi na muombaji kuwa anaweza kuwa mwizi, au mtu mbaya amekuja kwake kumpeleleza.

Nadhani katikati ya miaka ya 1990, hali ikaanza kubadilika baada ya mageuzi ya uchumi, huku watu binafsi wakiruhusiwa kufungua viwanda kwa ajili ya kujenga nchi na kuendeleza huduma kwa jamii, ndipo pamoja na mambo mengine viwanda vya maji ya chupa vikaanza.

Na hata kwenye miaka hiyo ni watu wachache tu ambao walionekana wenye uwezo ndiyo walionekana kumudu kununua na kuwa nayo.

Kwa sasa kila mmoja, hata mwananchi wa kawaida sana anaweza kumudu kununua maji kutokana na yeye mwenyewe anavyotaka, ziwe za chupa ndogo au kubwa kabisa. Na maji hayo huwa safi na salama. Ni kweli tumetoka mbali sana.

**Tuma meseji 0716 350534**







## M23 wagoma kuweka chini silaha

**GOMA,** DRC

WAASI wa M23 wanaoendesha harakati zao mashariki mwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wamekaidi agizo la usitishaji wa mapigano, wakisema suala hilo haliwahusu.

Agizo la kusitishwa mapigano na waasi hao kurudi sehemu waliyotoka lilitakiwa kuanza jana jioni.

Hata hivyo, waasi hao wametoa wito kwa serikali ya DRC kufanya nao mazungumzo ya moja kwa moja.

Msemaji wa M23, Lawrence Kanyuka, alisema kuwa kwa kuwa hawakuwa na wawakilishi katika mkutano huo uliofanyika nchini Angola, hawakujumuishwa katika mkataba.

"Sisi M23 sio Warundi, sio Wanyarwanda, sio Wakenya, na wala sio Waangola. Sisi ni Wacongo , na tuko nyumbani, wanatuambia tuondoke wapi ? Tunaondoka nyumbani kuelekea wapi ?" Munyarugerero alisema.

Viongozi waliotia saini mkataba huo ni kutoka Rwanda, DRC, Angola na Burundi.

Walisema chini ya usitishwaji wa mapigano, iwapo waasi hawataondoka katika eneo hilo kikosi cha kanda ya Afrika Mshariki kitayashambulia maeneo yao.

Serikali ya Kinshasa imekataa kufanya mazungumzo na M23, ikiwaita magaidi.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, inaishutumu Rwanda kuwaunga mkono waasi hao ambao wameteka eneo kubwa la jimbo la Kivu Kaskazini, mashariki mwa nchi hiyo.

Rwanda inakana kuhusika katika mzozo huo wa Congo. **BBC**

# Ukraine yakumbwa na giza, raia wateseka baridi kali

**KYIV,** UKRAINE

SEHEMU kubwa ya Ukraine imesalia bila umeme baada ya Russia kuishambulia kwa makombora gridi ya taifa. Hayo yanafanyika wakati wakazi wa mji wa Kyiv wametahadharishwa wajiandae kwa mashambulizi zaidi na wajihami kwa maji, chakula na nguo nzito.

Russia inakiri kwamba imeishambulia miundombinu ya umeme ya Ukraine kupunguza uwezo wa nchi hiyo kupambana na kuisukuma katika meza ya majadiliano. Ukraine, kwa upande wake, ilisema mashambulizi hayo ni uhalifu wa kivita.

Rais Volodymyr Zelenskiy pia aliituhumu Russia kwa kufanya msururu wa mashambulizi katika eneo la Kherson, mji ulio kusini mwa nchi hiyo ambao ulikombolewa kutoka mikononi mwa Russia mwezi huu.

Katika hatua nyingine, Kansela zamani wa Ujerumani, Angela Merkel ametetea sera yake dhidi ya Russia kabla ya nchi hiyo kuivamia Ukraine, akisema alikuwa ameishiwa madaraka ya kumshawishi Vladimir Putin.

Alisema alijaribu kuitisha mazungumzo ya Ulaya na Rais wa Russia na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron katika msimu wa joto wa 2021. Baada ya mihula minne Kansela Merkel, aliondoka madarakani mwezi Desemba na alitembelea Russia Agosti mwaka 2021.

Aliliambia jarida la habari la Ujerumani kwamba hisia ilikuwa wazi na kwa upande wa siasa za madaraka ulikuwa umekwisha.

"Putin na mamlaka pekee ndiyo yenye thamani muhimu katika mkutano wao wa mwisho, lakini Putin alimleta Waziri wa Mambo ya Nje Sergei Lavrov nikutane naye badala ya yeye mwenyewe," alisema.

Kutokana na uvamizi wa Russia, uliotanguliwa na wiki ya ukusanyaji mkubwa wa kijeshi kwenye mipaka ya Ukraine, wengi wamehoji kuwa Merkel na viongozi wengine wa Umoja wa Ulaya walipaswa kuwa na mtazamo mkali zaidi kwa nchi hiyo.

Mtaalamu wa sera za kigeni katika chama chake cha Christian Democrat (CDU), Mbunge Roderich Kiesewetter, ni miongoni mwa wale wanaosema alijua Putin anajaribu kugawanyisha na kudhoofisha Ulaya, lakini aliamini nguvu laini ndiyo njia sahihi.

Alidai kabla ya uvamizi, Ujerumani ilikuwa tegemezi kwa gesi ya Russia.

Katika mahojiano ya Spiegel, Merkel alisema msimamo wake kuhusu Ukraine katika mazungumzo ya amani ya Minsk umeifanya nchi hiyo kuwa na muda wa kujilinda dhidi ya jeshi la Russia.

Makubaliano ya kusitisha mapigano yalifikiwa mjini Minsk baada ya Russia kutwaa rasi ya Crimea mwaka 2014 na wakati wa vita vyake vya uwakilishi katika eneo la Donbas.

**NATO KUISAIDIA UKRAINE**

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kujihami ya NATO, Jens Stoltenberg, alisema jumuiya hiyo haitoacha kuiunga mkono Ukraine na haitosita kuipa misaada isiyo hatari. Akizungumza mjini Brussels jana kuelekea mkutano wa mawaziri wa mambo ya nje wa jumuiya hiyo utakaofanyika huko Bucharest wiki ijayo, Stoltenberg alisema NATO itaendelea kusimama na Ukraine na haitorudi nyuma. Mashambulizi ya Russia yamelaaniwa na marafiki wa Ukraine, lakini nchi hiyo inasema inalenga miundo mbinu inayohusishwa na jeshi.

Russia ilisema Ukraine inaweza kusitisha mateso wanayopitia raia wake iwapo tu itayakubali matakwa yake. **DW**



Waziri Mkuu mteule wa Malaysia, Anwar Ibrahim akiwapungia mkono wafuasi wake baada ya mkutano wake na waandishi wa habari mjini Sungai Long, Selangor, Malaysia, **PICHA: REUTERS**

# Uganda yafunga shule kukabiliana na ebola

**KAMPALA,** UGANDA

SERIKALI ya Uganda imezifunga shule zote nchini humo katika kukabiliana na kusambaa kwa ugonjwa wa Ebola.

Kutokana na hatua hiyo, mamilioni ya wanafunzi watarejea nyumbani baada ya shule kufungwa jana.

Hata hivyo uamuzi wa kufungwa kwa shule nchini kote wiki mbili kabla ya mwisho wa muhula, umechukuliwa ili kuzuia kuenea kwa Ebola wakati nchi hiyo ikiendelea kupambana na mlipuko huo.

Hatua hiyo pia imeleta ukinzani na msimamo rasmi wa serikali kwamba hali imedhibitiwa.

Katika miezi miwili iliyopita watu 55 walikufa na virusi hivyo na kuna uwezekano wa vifo 22 vya Ebola kabla ya mlipuko huo kutangazwa rasmi Septemba 20.

Baadhi ya wataalam walielezea kutoridhishwa kwao na hatua ya kufungwa kwa shule, wakisema kuwa kuwaweka wanafunzi ndani kwa wiki nyingine mbili itakuwa njia bora ya kukomesha kuenea kwa ugonjwa huo hatari.

Ebola ni maambukizi ya virusi ambayo husambazwa kupitia maji maji ya mwili wa mgonjwa. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KADI YA BAJAJI

**AHMED ISSA MAJURA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC SSU CAS – TVS KING.** Chassis namba **MD6M14PAJ4G43682.** Engine namba **AK4GJ4452666.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Control No. 9910833888911.**

## KUPOTEA KADI YA GARI

**THECLA WANKURU KOHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 286 ABF – LANDROVER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB /5452/2022.**

**SHERIA YA UMILKISHWAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUSUDIO LA KUTOHUISHA MILIKI YA ARDHI**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: ATANAS ZAKARIA NDANYOYE WA S.L.P 5035 MOROGORO**
**ARDHI:KIWANJA NA. 28 KITALU D MOROGORO TOWNSHIP (NKOMO STREET) MOROGORO**
**MUOMBAJI: ABDALLAH SAFAR** ambaye ni mrithi wa marehemu **ALLY ABEDI SAFAR WA S.L.P 37 MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **HATI YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imekwisha muda wake na ninakusudia kutokuhuisha miliki yake kwa aliyekua mmiliki wa kwanza ndugu **ALLY ABEDI SAFAAR.**
Zaidi sana ofisi inakusudia kumilikisha ndugu **ATANAS ZAKARIA NDANYOYE** ambaye ni mnunuzi wa kiwanja hiki wa **S.L.P 5035 MOROGORO**
Ambaye ndiye aliyeendeleza kiwanja hiki iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti MAELEZO yeyote yaelekezwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA YA MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO.**

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

## KUPOTEA KADI YA GARI

**YADON MTARIMA KOHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 230 ADE – LANDROVER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB /5452/2022.**

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 129 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late ZABELA CLEMENT KILAKATA**

**By 1. ASHA MANENO CHIWANGA**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **20th** day of **December / 2022.**
Dated at **Morogoro**, this **22nd** day of **OCTOBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 128 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late: LAZARO STEVEN BONZO**

**BY 1. MARY STELLA MAKENE BONZO**

**All persons** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 20TH DECEMBER.........2022
Dated at MOROGO this 22 day of NOVEMBER.........2022

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARY JACKSON MALEKO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S0266/0027** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **REGINAMUNDI GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka **2005.** Kwa yeyote atakaekiona

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 126 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late: EVA STANLEY MADINDA**

**BY 1. STANLEY LEONARD MADINDA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 1ST DECEMBER.........2022
Dated at MOROGO this 23RD day of NOVEMBER.........2022

RESIDENT MAGISTRATE

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, ni mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-7

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Adel huyu ndiyo mchumba wangu ambaye tunatarajia kuwa tutaoana Mungu akipenda."

"Vizuri sana." Akajibu huku akimsogelea na kumpa mkono.

"Mpenzi Enock, huyu ni yule mgeni niliyekuambia kuwa aliniokoa kwenye ajali ya bodaboda siku ile, anaitwa Adel...Adel nani vile..."

"Adel Adam." Mwenyewe akajibu huku bado mikono yake ikiwa imeshikana na ya Enock.

"Ooh, vizuri ahsante sana kwa msaada wako, wewe umehamia kwenye kijiji hiki?"

"Hapana, nilikuja huku kwa ajili ya kumchukua bibi yangu kumpeleka Dar kwa matibabu, lakini kwa bahati mbaya hali yake haikuwa nzuri ya kuweza kumchukua, hivyo kwa sasa anatibiwa kwenye kijiji jirani, halafu mimi niko hapa kuangalia kwanza afya yake hado hapo baadaye."

"Okay karibu sana kijijini kwetu." Enock akamkaribisha.

"Ahsante sana, nashukuru kupata mtu ambaye nitakuwa naye karibu kwa sababu karibuni mara zote niko peke yangu na mpweke sana."

"Hakuna shaka."

"Tena nina bahati baada ya kukutana na dada Mary siku ile ndiyo angalau nilikuwa napata mtu ambaye naweza kusimama naye na kuongea angalau kwa dakika mbili."

"Jamani eee, yaani kuwatambulisha mmezoeana ghafla mpaka mnanisahau mimi niliyewakutanisha?" Mary akatania na vicheko vikafuatia.

Mary ndiyo alikuwa mtu mwenye furaha kubwa moyoni na kujipa pongezi kwa kitu alichokifanya. Tayari alianza kusikia minong'ono kwa watu wakisema ana ana uhusiano na Adel wakati si kweli. Kwa kuweka mambo sawa akatengeneza mpango wa kuwakutanisha ili kama Enock na Adel wakiwa pamoja na marafiki, ule uvumi utakuwa umekufa kifo cha kawaida. Sasa atakuwa anaishi maisha ya amani na furaha.

**********************************

"Nimewaita hapa kwa kazi moja tu." Akaunguruma.

Aliongea maneno hayo mbele ya vijana wawili ambao walikuwa wamejaa miili. Vijana wa mjini waliwaita mabaunsa.



**"Kamwagiwa na Enock au na Mary?" Kijana mmoja aliwauliza wenzake aliokuwa amekaa nao chini ya mti wakicheza drafti.**

"Kuna kijana mmoja hapa kijijini anaitwa Adel. Nataka mfanye kazi moja ya kumkamata, kumtesa na kumlazimisha kuondoka hapa kijijini mara moja,"

"Siyo kumuua bosi?"

"Hapana, kumuua ni kosa kubwa la kiufundi. Si unajua hapa tumenunua ardhi kimagumashi, kwa hiyo hatutaki kumwaga damu ya mtu ambayo inaweza kuwalazimisha hata watu wasiokuwa na 'macho' wakaja kumulika huku kuna nini."

Alikuwa ni Mosha Usonzo akiwaelekeza moja ya vijana wake ambao amewaweka kijijini hapo kwa ajili ya usalama na kumlinda yeye na utajiri wake.

Bado Usonzo alikuwa na kinyongo na Adel. Hata aliposikia kuwa kijana huyo na Enock ni marafiki wakubwa kwa sasa bado alikuwa na wasiwasi.

Akajua kuwa huenda Mary ametumia njia hiyo ili mchumba wake asiwe na wasiwasi naye. Usonzo bado alikuwa anamhitaji Mary.

"Yule kijana amekuja hapa kwa ajili ya ugonjwa wa bibi yake bibi Anna Msafiri. Nimeambiwa kuwa alitoka Dar es Salaam kuja kumchukua akatibiwe huko, lakini alipofika akakuta hali yake ni mbaya kiasi kwamba haikuwezekana kumsafirisha kwa hiyo wanampeleka hospitali ya mkoani. Sasa hivi bibi ametoka na yupo vizuri, cha ajabu hadi leo yupo. Hataki kuondoka na kisa ni yule msichana. Mimi namtaka yeye hanitaki, lakini naona kama amemkubali yule kijana asiye na chochote." Usonzo akaongea kwa hasira kidogo.

"Bosi samahani kidogo, mbona naona kama kijana huyu si hatari sana kwako, huyo mchumba wake? Wewe si umataka? Wa kumfanyizia si mchumba wake tu. Huyu mwingine siyo mkazi wa huko, yeye si ataondoka tu?"

"Duh, Jaffar umeongea jambo la maana sana. Unajua sikutarajia kupata ushauri kama huo. Yaani hapa ni kwamba mtu wa kudili naye mimi ni Enock tu na si Adel."

"Ni kweli Adel ni mpita njia, hata akiondoka, umtishe, umuue, lakini si rahisi kumpata Mary kama Enock atakuwepo. Hapa anayetakiwa kufanyiwa kazi ni Enock."

"Sahihi kabisa, nimekuelewa na nitafanya hivyo, Enock kama hayupo kwenye mikono ya Mary, itakuwa rahisi kwangu kummiliki. Ila kwa hili ambalo nimelipanga sitoliahirisha kwa sababu lengo ni kumtisha tu Adel aondoke, na akiondoa nyayo zake kwenye kijiji hiki, sasa tutadili na Enock." Usonzo alielekeza mipango yake.

**********************************

Kijiji kiliamka na habari mpya. Ilikuwa ni ya kusikitisha kwa baadhi ya wanakijiji na baadhi ilikuwa ni kama sherehe.

"Kamwagiwa na Enock au na Mary?" Kijana mmoja aliwauliza wenzake aliokuwa amekaa nao chini ya mti wakicheza drafti.

"Kamwagiwa na Enock, si jamaa kajifanya kujipendekeza hadi kawa rafiki yake, kumbe anamchukulia mchumba wake, Enock akawafumania. Nasikia kamwagia maji ya betri machoni amekimbizwa kwenye hospitali ya mkoa. Akiona tena yule sijui."

Kijana mwingine akamtazama mwenzake, halafu akajibu. "Siyo hivyo nilivyosikia mimi. Ukweli ni kwamba jamaa kweli kamwagiwa sijui maji ya betri, sijui tindikali, lakini aliyemwagia ni Mary mwenyewe." Muulizaji na yule aliyeongea mara ya kwanza wote wakashtuka.

"Ndiyo, siyo kweli kwamba alikuwa mchumba wa Mary. Walikuwa marafiki tu wa kufagamiana na kuzoana. Yule jamaa alimuokoa Mary kwenye ajali ya bodaboda. Haiwezekani mwanamke akawa na mpenzi halafu akaenda kumkutanisha na mchumba wake, wakawa marafiki, si kweli tunadanganyana. Hakuwa mpenzi wake, ila nasikia jamaa baadaye akawa na tamaa, akaanza kumtongoza. Kila akimkatalia, jamaa analazimisha tu, mwanamke akawa anamuelewesha kuwa wewe ni rafiki ya mchumba wangu haelewi, akaona hali hii siku moja tutakuja kufumwa. Hivi tu kuna baadhi ya watu wanatufikiria vibaya, je tukifumwa, kwa hasira akamwagia tindikali."

Ilikuwa ni wakati huo huo msichana Ziada alikuwa anapita maeneo hayo na kuyasikia yote.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SIMBA QUEENS WAINGIA KAMBINI KUSAKA UBINGWA

Na Saada Akida

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens wameingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya ligi hiyo inayotarajiwa kuanza rasmi Desemba mwaka huu kuhakikisha wanatetea taji hilo.

Simba watafungua dirisha la ligi hiyo ikiwakaribisha JKT Queens katika uwanja wa Mo Simba Arena, mchezo utakaopigwa Desema 6, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana Meneja wa Simba Queens, Selemani Erassy alisema wanaendelea vizuri na maandalizi kuelekea msimu mpya wa ligi hiyo.

**Alisema baada ya mapumziko kikosi kimeingia kambini jana na kufanya mazoezi mara moja kwa siku na tumejiandaa vizuri kwa sababu ya ugumu wa ligi ya msimu huu.**

"Wachezaji wote wako fiti na wameingia kambini na kuendelea na maandalizi yetu ya ligi, msimu huu utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu ya kula timu inahitaji kufanya makubwa kama ilivyo kwa Simba," alisema Erasssy.

"Hatuna muda wa kupoteza sasa tunahitaji kuendelea na ufalme wetu katika ligi ya Tanzania kwa kocha wetu Charles (Lukulu) kusuka kikosi chake na kuwa bora zaidi," aliongeza.

Alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanatetea taji la ubingwa na wachezaji wanatambua na kuwepo kwa ari kubwa ndani ya timu hiyo.

Baada ya mchezo huo dhidi ya JKT Queens, Simba Queens itakuwa na kibarua kingine ugenini dhidi ya The Tiger Queens katika dimba la Black Rhino halafu wekundu wa Msimbazi hao watakuja kukutaa na Yanga Princess Desemba 22 mwaka huu, Dar es Salaam.



Mabondia Rashid Matumla (kulia) na Maneno Osward, wakitunishiana misuli wakati walipokuwa wanapima uzito kujiandaa na pambano maalum la kumpa zawadi Rais Samia Suluhu Hassan, litakalopigwa leo katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Polisi: Tutawatia mikononi Simba*

Na Shufaa Lyimo

BENCHI la ufundi la Klabu ya Polisi Tanzania limesema halihofii kukutana na timu ya Simba licha ya kuwa na wachezaji wengi wa Kimataifa, kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu watakaoucheza Novemba 27, Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Kocha mkuu wa timu ya Polisi, John Tamba alisema wamejipanga vema kukutana na wapinzani wao.

"Hatuhofii kukutana na timu ya Simba licha ya kuwa na wachezaji wengi wa Kimataifa," alisema Tamba.

Alisema baada ya kupoteza mchrzo wao uliopita dhidi ya Mtibwa Sugar kwa kukubali kichapo cha mabao 2-1 Morogoro, anaendelea kuyafanyia kazi makosa aliyoyabaini katika mchezo huo.

"Mpira ni mchezo wa makosa kuna makosa ambayo nimeyaona katika mchezo wetu uliopita ninayafanyia kazi na ninaamini hayawezi kujirudia katika mchezo huo na tunaomba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono," alisema.

Kocha huyo aliongez kuwa wachezaji wote wanaendelea vizuri na kudai hakuna mchezaji yeyote ambaye ni majeruhi.

Alisema morali ya kila mchrzaji ipo vizuri kuhakikisha hwaupotezi mchezo wao huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu.

## Yanga princess yatesti mitambo

Na Adam Fungamwango

TIMU ya soka ya wanawake, Yanga Princess jana iliichapa JKT Queens mabao 3-1 kwenye mechi ya kirafiki ikiwa ni maandalizi ya Ligi Kuu ya wanawake msimu wa 2022/23 itayotarajiwa kuanza Desemba 6, mwaka huu.

Mechi hiyo ilichezwa jana asubuhi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam huku mabao yote yakifungwa na wachezaji kutoka nchini Nigeria.

Mabao mawili yalifungwa na Wogu Chioma, huku moja likipachikwa na mwenzake, Precious Christopher.

Timu zote mbili zipo kwenye maandalizi ya Ligi Kuu Tanzania Bara,

JKT Queens itaanza kufungua ligi hiyo Desemba 6 itakapocheza dhidi ya Simba Queens kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam, huku Yanga Princess yenyewe itacheza kesho yake, Desemba 7 dhidi ya Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

## Town Classic, Waluguru kukinukisha Moro

Na Sabato Kasika

BENDI za Town Classic na Waluguru Original, zinatafanya maonyesha ya pamoja kwa siku mbili mfululizo kuanzia leo na kesho kama njia moja ya kuimarisha ushirikiano katika kufufua muziki wa dansi.

Meneja wa Town Classic Andrew Sekidia, alisema maonyesho hayo yatafanyoka mjini Morogoro, katika kumbi za Terminal Pub na F2 Florida na kisha wanamuziki watarudi Dar es Salaam kuendelea kuandaa nyimbo mpya.

"Ijumaa kampeni yetu ya Mo Green ilikuwa imeandaa mashindano ya ngumi katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, bendi zetu ziliporomosha muziki na sasa tutafanya maonyesho mengine leo na kesho," alisema Sekidia.

Mkurugenzi wa bendi ya Waluguru Original yenye maskani mjini Morogoro, Killer alisema hatua hiyo inaonyesha kuiwa sasa bendi ya Dar es Salaam zimetambua kwamba hata bendi za mikoani ziko vizuri.

"Zamani bendi ya Dar es Salaam zilikuwa hazina ushirikiano za mikoani, lakini sasa tunashirikiana vizuri, kwani zimekuwa zikija nyingi Morogoro na kushirikiana nasi na sasa wamekuja Town Classic," alisema Killer.

Killer alisema njia hiyo ya kufanya maonyesho ya pamoja, inaweza kurejesha hadhi ya muziki wa dansi ambayo imepotea na kusababisha baadhi ya bendi kufa au kubaki zikisuasua kwa kukosa mashabiki.

"Sisi tunafurahi tunapoona bendi zinakuja Morogoro kufanya maonyesho, kwani mji huu na mkoa kwa ujumla ni chimbuko la wanamuziki wengi waliowahi kutamba katika dansi," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO AWINDWA SAUDIA

KLABU ya Al-Hilal ya Saudi Arabia inaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37. (***Sky Sports***)

### HATAKIWI MADRID

REAL Madrid imesema "haitakuwa na maana katika mradi wetu wa michezo" kumrejesha Cristiano Ronaldo katika klabu kwa kipindi hiki. (***AS***)

### SILVA ANAAMINI

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva anaamini kuwa mchezaji mwenzake wa Ureno, Cristiano Ronaldo amethibitisha kuwa bado anaweza kucheza katika kiwango cha juu baada ya kuweka historia ya Kombe la Dunia. (***Mirror***)

### TROSSARD ATAKIWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea iko tayari kufanya mazungumzo na mshambuliaji wa Ubelgiji, Leandro Trossard mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake na Brighton unamalizika msimu ujao. (***Football Insider***)

### WOODWARD KUWA MSHAURI

ALIYEKUWA makamu mwenyekiti mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward amefuatwa na makundi yanayotaka kuinunua klabu hiyo na kumtaka awe mshauri. (***Mail***)

### LUKAKU KUONGEZA MWAKA

KLABU ya Inter Milan itaongeza muda wa mkopo wa mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, kwa mwaka mwingine. (***Sky Sport***)

### ARTETA AWANIWA BARCA

ARSENAL ina wasiwasi wa kumpoteza kocha wake, Mikel Arteta mwenye umri wa miaka 40, huku Barcelona wakidhamiria kumfanya mchezaji wao wa zamani kuwa kocha wao wa baadaye. (***Sport***)

### RABIOT ATAKA MKATABA

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 27 amesema Kombe la Dunia linaweza kumsaidia kupata mkataba mpya katika klabu ya Juventus, ambapo mkataba wake wa sasa unaisha msimu wa joto, au kuhamia kwingine. (***La Repubblica***)

### MOUKOKO KUONDOKA DORTMUND

KLABU kadhaa zinaamini kuwa mshambuliaji wa Ujerumani, Youssoufa Moukoko mwenye umri wa miaka 18, yuko tayari kuondoka Borussia Dortmund mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. (***90 Min***)

### BOUNOU AWINDWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inamfuatilia mlinda mlango wa kimataifa wa Morocco anayeichezea Sevilla Yassine Bounou mwenye umri wa miaka 31. (***Football Insider***)

### RODRYGO KULIPA FIDIA

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid raia wa Brazil, Rodrygo mwenye umri wa miaka 21, huenda akalazimika kulipa kipengele cha kusitishwa mkataba wake cha euro milioni 7 baada ya kutengana na wakala wake, Nick Arcuri. (***Sport***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RICHARLISON: NIMEFUNGA BAO ZURI ZAIDI MAISHANI

**DOHA,** Qatar

**Ni baada ya kuiongoza Brazil kuibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Serbia na...**

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Richarlison amesema bao la pili alilofunga dhidi ya Serbia kwenye ushindi wa 2-0 katika kombe la Dunia Alhamisi, ni mojawapo ya magoli mazuri zaidi aliyowahi kufunga katika maisha yake ya soka.

Kocha Tite alikuwa na wakati mgumu kuchagua mshambuliaji anayeanza, lakini alifurahishwa na uchezaji wa Richarlison baada ya kufunga mabao yote mawili ya Brazil katika ushindi wao huo.

Richarlison alifunga bao la kwanza akicheza namba tisa mbele ya Gabriel Jesus wa Arsenal na Pedro wa Flamengo, na baada ya kipindi cha kwanza bila bao, alifunga la kwanza dakika ya 62 baada ya kombora la Vinicius Junior kupanguliwa na kumkuta yeye.

Na dakika 10 tu baadaye alifunga bao zuri kwa tikitaka ambalo linaweza kuwaniwa kuwa bao bora la michuano akiunganisha krosi ya Vinicius.

Lilikuwa ni bao lake la 19 la kimataifa, na baada ya mchezo huo Richarlison alisema anaamini linaweza kuwa bora kwake.

**"Lilikuwa bao zuri," aliwaambia wanahabari. "Labda moja ya mazuri zaidi katika uchezaji wangu hadi sasa.**

"Ni Kombe la Dunia, ilikuwa mechi ngumu ... ilikuwa moja ya mabao mazuri ambayo nimewahi kufunga."

Nae Tite akizungumza jinsi ilivyokuwa ngumu kuchagua mshambuliaji wa kwanza alisema alifurahishwa na Richarlison.

"Lazima niwaambie, nilikuwa na majina sita au saba ya kuwaita (kama mshambuliaji), na yeyote niliyempigia simu, tungekuwa na timu kubwa," Tite alisema.

"Kwa hiyo tulikuja na Pedro, Richarlison na Gabriel. Tungekuwa na (Gabriel) Barbosa, tungekuwa na Firmino, tungekuwa na (Matheu) Cunha, tungekuwa na Hulk.

"Richarlison ni mzuri, tunaona jinsi anavyodhibiti mpira ... katika kipindi cha pili aliunda kasi kubwa, alirekebisha, alitulia kidogo, alikuwa sahihi zaidi katika pasi zake.

"Mguso wa kwanza wa mpira ni muhimu ili kuufanya utiririke, na kisha akaanza na kiasi."

Brazil wataendelea na kampeni zao katika Kundi G Jumatatu watakapomenyana na Uswizi, kabla ya kufunga hatua ya makundi dhidi ya Cameroon Ijumaa ijayo.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,053,2
MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
MBEYA CITY
1 | 1.19
X | 5.47
2 | 12.71
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LUKAKU HANA UHAKIKA KUIVAA MOROCCO

**DOHA,** Qatar

ROMELU Lukaku hana uwezekano wa kuanza mechi ya pili ya Ubelgiji Kombe la Dunia dhidi ya Morocco licha ya kurejea kwenye mazoezi ya timu kwa mujibu wa kocha mkuu, Roberto Martinez.

Lukaku amecheza mechi tano pekee akiwa na Inter Milan katika msimu ambao ulikuwa na majeraha na hakuwepo kwa kikosi cha Ubelgiji kikianza kampeni ya Kundi F kwa ushindi mgumu wa 1-0 dhidi ya Canada Jumatano.

Huku Martinez akitumaini mfungaji bora wa muda wote wa Ubelgiji atarejea dhidi ya Morocco kwenye Uwanja wa Al Thumama Jumapili, mshambuliaji huyo wa Nerazzurri anaweza kulazimika kukaa benchi.

"Leo (juzi), alifanya mazoezi, sasa tutaona jinsi mwili wake utakavyofanya," alisema kocha huyo. "Sidhani kama yuko tayari kucheza na Morocco tangu mwanzo, lakini tutagundua hilo katika siku mbili zijazo.

"Lakini anaonekana anaendelea vizuri, na nina furaha kumuona tena kwenye mazoezi ya kikundi."

Iwapo Ubelgiji itawashinda vijana wa kocha Walid Regragui mara nyingine, watakuwa timu ya kwanza katika historia ya Kombe la Dunia kushinda mechi tisa mfululizo za makundi kwenye michuano hiyo.

Ubelgiji pia hawajashindwa katika mechi zao nne zilizopita za Kombe la Dunia na timu za Afrika (walishinda tatu, sare moja), wakishinda Tunisia 5-2 katika mchuano wao wa mwisho mwaka 2018.

# *Ronaldo ajivunia kuweka rekodi Kombe la Dunia*

**DOHA,** Qatar

CRISTIANO Ronaldo amesema mustakabali wake wa klabu "haujalishi" baada ya "wakati mzuri" ambao ulimfanya kuweka rekodi kwenye Kombe la Dunia.

Nyota huyo alifunga kwa mkwaju wa penalti katika ushindi wa 3-2 wa Ureno dhidi ya Ghana katika mechi ya kwanza ya Kundi H kwenye Uwanja wa 974 na kuwa mchezaji wa kwanza kufunga katika michuano mitano tofauti ya Kombe la Dunia.

Vyombo vya habari vilitawala habari zake bada ya Ronaldo kukubali kusitisha mkataba wake na Manchester United, Jumanne kufuatia mahojiano makubwa na Piers Morgan ambapo alimkosoa kocha, Erik ten Hag, familia ya Glazer na wachezaji wenzake kadhaa wa zamani.

Kwa hiyo, Ronaldo hana klabu lakini, ingawa maswali juu ya mustakabali wake yataendelea kutawala mazungumzo, lengo lake la moja kwa moja linabaki katika kuichezea nchi yake huko Qatar.

"Ilikuwa ni wakati mzuri, Kombe langu la tano la Dunia. Tulishinda, tulianza (kwa mguu wa mbele), ni ushindi muhimu sana," aliuambia mkutano wa waandishi wa habari baada ya mechi.

"Tunafahamu kuwa katika mashindano haya mechi ya kwanza ni muhimu, lakini pia rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga katika michuano mitano ya Kombe la Dunia, ni jambo ambalo linanifanya nijivunie sana na nimefurahi sana timu imepata matokeo kwenye mchezo mgumu.

"Hatua muhimu zaidi ni kwamba tulishinda. Tulishinda, ningeweza kuisaidia timu yangu na mengine yote hajalishi."

Ronaldo pia alisifiwa na kocha mkuu, Fernando Santos, ambaye anaamini fowadi huyo atasalia kuwa gumzo miongoni mwa mashabiki wa soka kwa miongo mingi ijayo.



"Yeye ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani, hakuna shaka kuhusu hilo, mmoja wa wachezaji bora kabisa," alisema.

"Cristiano ni jambo la ajabu, gwiji, kama wengine wengi waliokuja na kuondoka katika soka. Katika muda wa miaka 50, tutaendelea kumzungumzia."

Ureno inaweza kutinga hatua ya 16 bora kwa ushindi dhidi ya Uruguay siku ya Jumatatu, na hatua ya makundi itakamilika dhidi ya Korea Kusini siku nne baadaye.

232,366/-

# IRAN YACHANA MKEKA WA WALES

**DOHA,** Qatar

USHIRIKI wa kombe la Dunia la kwanza kwa Wales kwa kipindi cha miaka 64 unaonekana kuelekea kumalizika kwa machungu baada ya kipigo cha kuhuzunisha cha mabao 2-0 kutoka kwa Iran, jana.

Mchezaji wa akiba Rouzbeh Cheshmi alifunga kwa umbali wa yadi 20 zikiwa zimesalia dakika tisa mchezo kumalizika, kabla ya Ramin Rezaeian kumaliza shambulizi la kushitukiza dakika za nyongeza na kuipatia ushindi timu iliyofufuka ya Iran, ambayo imeongeza matumaini ya kutinga hatua ya mtoano wa 16 bora kwa mara ya kwanza katika historia yao.

**Hilo lilikuwa pigo kali kwa matarajio ya Wales, ambayo ilimpoteza golikipa wake Wayne Hennessey aliyetolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya Medhi Taremi.**

Kama walivyofanya kwenye sare ya kwanza dhidi ya Marekani, Wales walianza vibaya na kwa kufungwa bao la mapema na mchezaji Ali Gholizadeh ambalo lilikataliwa na VAR baada ya kuonekana ameotea.

Safari hii wachezaji wa Iran waliimba wimbo wao wa taifa wakati wakiwa wamekataa kufanya hivyo wakati walipofungwa na England.

Wakishangiliwa na umati wa watu wenye shauku na karibu wote wa Irani, vijana wa kocha, Carlos Queiroz hawakubahatika sana kufunga bao mapema katika kipindi cha pili, wakati Sardar Azmoun na Gholizadeh wote waligonga nguzo ndani ya sekunde chache.

Wales sasa wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kuhitaji kushinda mechi yao ya mwisho ya kundi Jumanne dhidi ya England.



Waimbaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri, Usharika wa Kinyerezi, wakicheza katika uzinduzi wa albamu mbili za mwimbaji wa nyimbo hizo, Lilian Naman uliofanyika kanisani hapo Jumapili iliyopita. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wachezaji Simba wawekwa kitimoto

INATOKA UKURASA 32

Alisema mechi kama hizi ambazo unakwenda kucheza na timu ambazo zinakamia inabidi pia na wachezaji wao iwalazimu kuongeza nguvu ili kupata matokeo mazuri.

Kwa sasa wanachama na mashabiki wa Simba wamekuwa hawana furaha na timu yao kutokana na si tu kupata matokeo yasiyoridhisha, lakini hata kiwango kimekuwa si cha kuridhisha, ari ya upambanaji wa wachezaji ukiwa umepotea, na vile vile kuonekana kupungua kwa viwango vya baadhi ya wachezaji wa timu hiyo.

## *Yanga SC, Mbeya City mechi ya kiwango leo*

INATOKA UKURASA 32

Shooting ikiwakaribisha Singida Big Stars katika uwanja wa Uhuru saa 10:00 alasiri.

Ruvu wanashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kupoteza kwa mabao 4-0 dhidi ya Simba.

Kuelekea mchezo wa leo, Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Rajab Mohammed alisema wamejiandaa vizuri na mchezo wao dhidi ya Singida Big Stars kuhakikisha wanapata matokeo mazuri yenye alama tatu.

"Tulifanyia kazi mapungufu yetu yaliyojitokeza katika mchezo uliopita dhidi ya Simba na tuko imara kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu dhidi ya Singida Big Stars nyumbani," alisema Kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans Van Pluijm alisema wamefanya mazoezi ya mwisho asubuhi na wamejiandaa na wako tayari kwa mchezo huo.

"Tumekuja kutafuta pointi muhimu katika mchezo huu dhidi ya Ruvu Shooting, tumejiandaa kwa asilimia 100 kupambana kusaka ushindi, utakuwa mchezo mgumu kwa kila mmoja wetu kuhitaji alama muhimu," alisema Pluijm.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/11/22 | 18:00 | Walsall FC vs Carlisle United | 2.28 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/11/22 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Chesterfield FC | 2.44 | 3.35 | 2.75 |
| 03. 26/11/22 | 18:00 | Shrewsbury Town vs Peterborough United | 3.10 | 3.25 | 2.27 |
| 04. 26/11/22 | 18:00 | Hartlepool United vs Harrogate Town | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 05. 26/11/22 | 20:00 | Dagenham and Redbridge FC vs Gillingham FC | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 06. 26/11/22 | 20:00 | SC Pisa vs Ternana Calcio | 2.21 | 3.30 | 3.20 |
| 07. 26/11/22 | 20:30 | Albacete Balompie vs Racing Santander | 2.27 | 3.05 | 3.30 |
| 08. 27/11/22 | 13:30 | Ankara Keciorengucu vs Samsunspor | 2.48 | 3.35 | 2.75 |
| 09. 27/11/22 | 13:30 | Pendikspor vs Eyupspor | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 10. 27/11/22 | 16:00 | Burgos CF vs Real Zaragoza | 2.48 | 2.90 | 3.10 |
| 11. 27/11/22 | 16:00 | Erzurumspor FK vs Bandirmaspor | 2.34 | 3.35 | 2.90 |
| 12. 27/11/22 | 17:00 | Como 1907 vs SSC Bari | 2.85 | 3.20 | 2.46 |
| 13. 27/11/22 | 17:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Ascoli Calcio 1898 | 2.40 | 3.15 | 3.00 |
| 14. 27/11/22 | 18:00 | CD Leganes vs Granada CF | 2.55 | 3.00 | 2.90 |
| 15. 27/11/22 | 20:00 | Palermo FC vs Venezia FC | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 16 27/11/22 | 20:00 | FC Cartagena vs SD Eibar | 2.38 | 3.10 | 3.05 |
| 17. 27/11/22 | 22:00 | Spain vs Germany | 2.50 | 3.25 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 26/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2915 | Tunisia vs Australia | 2.11 | 3.19 | 3.54 |
| 13:30 | 4454 | Tuzlaspor vs Yeni Malatyaspor | 1.92 | 3.46 | 3.46 |
| 14:00 | 2525 | Hebei Zhongji vs Hangzhou NG | 29.35 | 15.65 | 1.01 |
| 14:00 | 3580 | Muang Thong Utd vs Bangkok Utd | 3.17 | 3.31 | 2.07 |
| 14:00 | 3724 | Oliveirense vs CD Feirense | 2.37 | 3.10 | 2.81 |
| 14:30 | 3373 | Shenzhen vs Wuhan Three Towns FC | 58.41 | 11.68 | 1.01 |
| 14:30 | 4112 | Guangzhou Evergrande vs Henan Jianye | 9.18 | 5.08 | 1.26 |
| 15:00 | 3711 | Tianjin Teda vs Shanghai SIPG | 5.06 | 3.90 | 1.55 |
| 15:00 | 4637 | Nzoia United vs Bandari | 3.35 | 3.00 | 2.29 |
| 15:30 | 3072 | ZR Temouchent vs JS Bordj Menaiel | 2.49 | 2.95 | 3.05 |
| 15:30 | 5495 | US Chaouia vs NA Hussein Dey | 1.61 | 3.45 | 5.25 |
| 16:00 | 1516 | FC Muza vs Nkwazi | 2.65 | 2.50 | 3.40 |
| 16:00 | 1603 | Poland vs Saudi Arabia | 1.74 | 3.55 | 4.70 |
| 16:00 | 1715 | Etincelles vs Rutsiro FC | 2.28 | 2.78 | 3.31 |
| 16:00 | 2353 | Sunrise vs Bugesera FC | 2.23 | 2.82 | 3.36 |
| 16:00 | 2434 | Police FC Rwanda vs Gorilla FC | 1.78 | 3.25 | 4.37 |
| 16:00 | 3748 | Napsa Stars vs Nkana FC | 2.72 | 2.43 | 3.11 |
| 16:00 | 4562 | Ruvu Shooting vs Singida BS FC | 2.93 | 2.69 | 2.59 |
| 16:00 | 5172 | Bidco United vs Gor Mahia | 3.46 | 2.82 | 2.19 |
| 16:00 | 5457 | Kabwe Warriors vs Green Buffaloes | 2.59 | 2.69 | 2.93 |
| 16:00 | 5937 | Boluspor vs Sakaryaspor | 1.80 | 3.41 | 4.00 |
| 16:30 | 5310 | Gaborone United vs Township Rollers | 2.74 | 3.08 | 2.44 |
| 17:00 | 1026 | Parma vs Modena | 1.88 | 3.42 | 3.92 |
| 17:00 | 2942 | Slovan Liberec vs Sigma Olomouc | 2.18 | 3.22 | 3.02 |
| 18:00 | 4150 | Sheffield Wed vs Mansfield | 1.45 | 4.24 | 6.31 |
| 18:00 | 4342 | Portsmouth vs MK Dons | 1.82 | 3.46 | 4.06 |
| 18:00 | 4666 | Barnsley vs Crewe | 1.41 | 4.35 | 6.73 |
| 18:00 | 5221 | Oxford Utd vs Exeter | 1.99 | 3.50 | 3.36 |
| 18:00 | 5432 | Shrewsbury vs Peterborough | 3.06 | 3.21 | 2.24 |
| 18:00 | 5835 | Cambridge Utd vs Grimsby | 2.28 | 3.25 | 2.95 |
| 18:15 | 2652 | Young Africans vs Mbeya City | 1.19 | 5.47 | 12.71 |
| 18:15 | 4461 | Malaga vs Ponferradina | 2.20 | 3.13 | 3.28 |
| 18:15 | 4607 | Alaves vs Villarreal B | 1.68 | 3.57 | 4.86 |
| 18:30 | 1841 | Al Sharjah SC vs Baniyas | 1.37 | 4.57 | 6.61 |
| 19:00 | 2710 | France vs Denmark | 1.75 | 3.56 | 4.62 |
| 19:00 | 3574 | Genclerbirligi vs Caykur Rizespor | 3.60 | 3.36 | 1.91 |
| 19:30 | 2355 | AS Douanes vs Generation Foot | 3.60 | 2.55 | 2.50 |
| 19:30 | 2506 | Teungueth vs ASC Linguere | 2.13 | 2.85 | 4.00 |
| 19:30 | 3338 | ASC Jaraaf vs AS Dakar Sacre Coeur | 1.78 | 3.06 | 4.76 |
| 20:00 | 1568 | AEK Larnaca vs Apollon Limassol | 2.14 | 3.24 | 3.39 |
| 20:00 | 2131 | FC Thun vs FC Vaduz | 1.86 | 3.69 | 3.45 |
| 20:00 | 3223 | Dagenham and Redbridge vs Gillingham | 2.55 | 3.09 | 2.70 |
| 20:00 | 5589 | Pisa vs Ternana | 2.15 | 3.28 | 3.23 |
| 20:15 | 3782 | Dodoma FC vs Namungo | 2.37 | 2.67 | 3.30 |
| 20:30 | 3877 | Real Oviedo vs Mirandes | 2.05 | 3.11 | 3.71 |
| 20:30 | 5365 | Albacete Balompie vs Racing Santander | 2.21 | 3.02 | 3.37 |
| 21:45 | 1062 | Sporting Braga vs CD Trofense | 1.09 | 9.38 | 22.94 |
| 22:00 | 4020 | RSC Anderlecht Futures vs Kfco Wilrijk | 3.10 | 3.69 | 2.04 |
| 22:00 | 4926 | Argentina vs Mexico | 1.55 | 3.95 | 5.80 |
| 23:45 | 4904 | Benfica vs Penafiel | 1.09 | 9.38 | 22.94 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Novemba 26, 2022

Nipashe




Iran yachana mkeka wa Wales UKURASA 31



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini. **PICHA: YANGA**

# Yanga SC, Mbeya City mechi ya kiwango leo

## ●●● Wanajangwani wakamia kuendeleza rekodi, Mbeya waahidi kuwatibulia mazima...

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga leo wanashuka dimbani kuendelea walipoishia katika kuhakikisha hawapotezi mechi wakati watakapowavaa Mbeya City.

Mchezo huo utakaopigwa katika dimba la Benjamin Mkapa Dar es Salaam utaanza majira ya saa 1:00 usiku.

**Yanga wanashuka dimbani wakiwa na rekodi ya kutopoteza mechi 48 ambapo leo wanahitaji kupata matokeo mazuri ya ushindi ili kufikisha mechi 49 katika Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Taarifa njema kwa mashabiki wa Yanga ni kurejea kwa kiungo mshambuliaji wa Wanajangwani hao, Stephane Aziz Ki aliyemaliza adhabu yake aliyopewa na Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ligi kwa kukosa michezo mitatu.

Azizi Ki 'mzee wa mipira iliyokufa' alikosekana katika michezo mitatu ya ligi hiyo baada ya kutumikia adhabu na sasa ataonekana katika kikosi cha timu hiyo endapo Kocha Mkuu, Nesreddine Nabi akimuweka katika mipango ya mchezo huo.

Wao Mbeya City wanashuka dimbani baada ya kupata pointi moja katika uwanja wa nyumbani dhidi ya Simba, huku wakidhamiria kutafuta pointi muhimu ugenini.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema muda mfupi wa maandalizi, waliwekeza sana katika mazoezi mepesi na wamejiandaa vizuri kukabiliana na Mbeya City.

Alisema Mbeya City wamekuwa wakiwapatia changamoto kubwa kwa sababu msimu uliopita walitoka nao sare katika uwanja huo wa Mkapa na anaimani mchezo wa leo utakuwa wa ushindani mkubwa.

"Kesho (leo) tutakuwa na mabadiliko katika kikosi chetu kulingana na mechi iliyopo mbele yetu, kuna wachezaji ambao wamerejea kikosini akiwemo Aziz Ki na kipa Djigui Diarra ambaye ametoka katika majukumu ya kitaifa," alisema Kaze.

Alisema wamejiandaa kukabiliana na wapinzani wao hao kwa kucheza mpira mzuri na kuwa makini na safu yao ya ushambuliaji akiwemo Tariq Seif, Isabilo na Paul Nonga ambao wamekuwa ni hatari.

"Tunaenda kucheza kwa heshima kubwa sana dhidi ya wapinzani wetu hao kwa sababu msimu huu wamejiandaa vizuri na kubadili benchi la ufundi kwa kuwepo kocha mwingine," aliongeza Kaze.

Naye Kocha Msaidizi wa Mbeya City, Anthony Mwamlima alisema wamekuja kushinda na kuleta changamoto dhidi ya Yanga na kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo wao wa leo.

"Matokeo ya mechi iliyopita na Simba tulipata pointi moja, tutaingia na mbinu mpya kabisa ya kukabiliana na Yanga, tutawaheshimu wapinzani wetu kutokana na ubora wa wachezaji wao, nina imani tutaenda kupata matokeo chanya," alisema Mwamlima.

Katika mchezo mwingine utakaopigwa leo Dar es Salaam mapema, Ruvu

INAENDELEA UK. 31

# Wachezaji Simba SC wawekwa kitimoto

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuonekana hawana ari ya upambanaji, hasa wakicheza kwenye viwanja vya ugenini, uongozi wa klabu ya Simba umewaweka kikao wachezaji wao na kuwakumbusha juu ya kile ambacho wanapaswa kufanya kwa ajili ya kuitetea nembo na kuwapa furaha wanachama na mashabiki wa timu hiyo ambayo kwa sasa imepotea.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amekiri kuwa mambo ni magumu na kwa sasa wa kuiokoa klabu hiyo ni wachezaji kupambana kwa ajili ya wanachama na mashabiki.

Kesho Simba itaingia kwenye Uwanja wa Ushirika Moshi kucheza dhidi ya Polisi Tanzania, baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

"Tumejitathmini baada ya mchezo dhidi ya Mbeya City, ile hali ilitutisha kwa kweli, kwa sababu tumekuwa hatuna matokeo ya kuaminika mikoani au ugenini," alisema Ally.

"Kwenye mechi tano tumeshinda moja, tumefungwa moja na sare tatu, haya ni matokeo mabovu. Timu inayosaka ubingwa haiwezi kupata matokeo ambayo sisi tunayapata," aliongeza kusema.

"Kwa hiyo imetushtua, tumefanya tathimini na kuzungumza na wachezaji wetu juu ya kile ambacho wanapaswa kufanya. Mambo ni magumu watu pekee wa kutuokoa ni wachezaji wetu kuingia na mbinu nyingine mbadala ya kujituma, ukweli tuseme hakuna timu iliyotuzidi kimbinu zaidi ya hali ya upambanaji."

Kuhusu mechi ya kesho, alisema maandalizi yalianza mara baada ya kumalizika kwa mechi dhidi ya Mbeya City.

"Kwa sasa kila kitu kinakwenda vizuri kwa ajili ya mechi hiyo. Itakuwa ni mechi ngumu, pamoja na kwamba imekuwa haipati matokeo mazuri sana msimu huu lakini tutegemee Polisi Tanzania tofauti kabisa, itaingia kwa kupambana ikiwa na ari, wataangalia aina ya matokeo waliyonayo kwa sasa wataingia kupata kutuzuia."

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >